# *Uwekezaji*

Hebu tuendelee tu kusimama kwa muda mfupi tu, wakati tukizungumza na Yeye sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu.

2 Baba yetu wa Mbinguni, kwa kweli tuna shukrani kwa ajili ya wakati huu tena kwamba tunaweza kusimama kuileta Injili kwenye jiji hili, Chikago, kama ilivyo mioyoni mwa hawa watu hapa, hawa Wakristo, kuona watu wao wameokoka. Pia, Baba, tunajua kwamba hakuna mtu anayeweza kuja isipokuwa Wewe umemvuta kwanza, Yesu alisema hivyo. Nasi tunaamini kwamba, kila mbegu iliyokusudiwa tangu zamani iliyo katika jiji hili sasa, hakuna njia ya kuwazuia wasiione Nuru ya Injili. Wewe utaninii, Wewe utalijalia hilo, Bwana. Utaiangalia, kuhakikisha inafika kule. Unauleta Ujumbe, nami ninaamini kwamba Wewe unaweza, na utawaleta wale kwenye Nuru ya Injili ambao Wewe umewakusudia kuiona.

3 Kwa hiyo, Baba, tunapoiacha Nuru yetu iangaze, na kutia jitihada zetu, katika vyote ambavyo tunajua jinsi, ku—kuleta ninii. . .Injili hii kuu ya wakati wa jioni; mawimbi ya dhambi kweli yanaingia, kutokuamini kila mahali. Loo, mambo mengi sana ya kutisha yakitukabili usoni mwetu. Bali tuna hakikisho la ninii. . ."Adui anapokuja kama mafuriko, Neno la Mungu litainua kiwango dhidi yake," Baba, na Wewe uliahidi hilo, kwa hiyo tunakushukuru Wewe.

4 Na sasa, leo hii, tusaidie tunapotulia sasa. Ninakushukuru kwa ajili ya yubile ya asubuhi, hizi nyimbo za ajabu na shuhuda, yoyote ambayo yamefanyika. Na sasa jalia tuliangalie Neno Lako, Bwana, kuvuta kutoka kwenye Hili, nguvu kwa ajili ya siku hii. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

5 Mwaweza kuketi. Asanteni, sana, kwa ajili ya mwaliko mwema wa kuja kuwa hapa pamoja nanyi. Na sasa ninataka kumshukuru maskini mama huyu hapa kwa ajili ya wimbo wake, jinsi ulivyokuwa wa ajabu. Ninaamini ilikuwa mara ya kwanza nimewahi kumsikia akiimba. Halafu basi, bila shaka, Ndugu yetu Mel Johnson pale, niliomba kwamba aimbe wimbo huo, wakati, *Nikumbuke Mimi*. Nasi tunao huko nyumbani, nami ninataka kuupata upya.

6 Naye Billy Paul, nafikiri, yeye huishi tu juu ya nyimbo hizo. Alizitia kwenye ninii. . .wakati zikiwa ofisini, na daima kuucheza kila mara kwa ajili ya watu ambao wanakuja na kuondoka, kutoka kote ulimwenguni. Nawe unaweza kuja karibu na ofisi na unaweza kumsikia Mel Johnson akiimba mara nyingi sana karibu hapo, kwenye kanda. Na basi wakati kwa namna fulani ninapoanza kujisikia mchovu na nimechoka, ni—nitashuka na kuketi mahali fulani katika chumba, na

kuzungumza tu. . .ninaleta kimoja cha spika, na kuusikiliza tena.

7 Kwa hiyo tu—tunashukuru sana kwa waimbaji hawa hodari. Nami ninawazia wakati tutakapouvuka mto huu wa Yordani. Ninataka kuisikia sauti hiyo tamu mno ya Mel Johnson ikiingiana na Einar Eckberg na wengi wa hao waimbaji mashuhuri ambao wamevuka mto. Kwa hiyo tunatazamia wakati huo.

8 Ninataka kumshukuru rafiki yangu mwema hapa, Dk. Lee Vayle, aliyekuwa mhudumu wa Kibaptisti, mwanachuoni hodari sana na mtu wa ajabu, ambaye amesimama mbele zangu juma hili na ameileta huduma kwa mtindo wake wa kufanya hivyo, akanipa usaidizi mkubwa hapa mkutanoni.

9 Wakati tunapokuwa na ibada hizo, maombi kwa ajili ya wagonjwa, tunaiita "ibada ya uponyaji," mara nyingi, mbele tu ya watu. Lakini, bila shaka, tunatambua kwamba hatuwezi kuwaponya watu, kwa urahisi tunawaombea tu watu.

10 Mtu fulani alisema, wakati fulani uliopita, kasema, "Ndugu Branham, ulimponya *nanii*?"

11 Nikasema, "Kamwe sikumponya mtu yeyote, maishani mwangu. Bali nimekuwa na majibu ya moja kwa moja ya maombi, kwa kuwa Yesu aliliahidi, na mimi—mimi ninaamini hilo."

12 Ninakumbuka ule usiku ambao ile—ile picha ya huyu Mwenye uhai mkuu, Roho Mtakatifu; ambapo kutoka Kutoka 13:22, ninaamini, ama 21, ambapo "Nguzo ya Moto itakutangulia, kukuongoza njiani," na jinsi Nguzo hiyo ya Moto ambayo ilikuwa pamoja na Musa, Hiyo iliwatungulia.

13 Halafu basi wakati ilipodhihirishwa hapa katika Mtu aitwaye Yesu, ambaye alikuwa Mwana wa Mungu. Halafu basi Yeye alisema Yeye alitoka kwa Mungu na kurudi kwa Mungu.

14 Ndipo baada ya kurudi Kwake, baada ya kupaa juu, jinsi lilivyokuwa ni jambo kuu kwa Mtakatifu Paulo, kabla hajakuwa Mtakatifu Paulo, alipoangushwa chini. Sasa, yeye akiwa ni Myahudi, kwa vyovyote asingeiita hiyo "Bwana." "Bwana, ungetaka nifanye nini?" Mnaona? Lakini yeye alijua kwamba Hiyo ilikuwa ni ile ile Nguzo ya Moto ambayo ilikuwa imewafuata watu wake, ama kuwaongoza watu wake. Hiyo ndiyo sababu aliita Hiyo, "Bwana, ungetaka nifanye nini? Na U Nani Wewe?"

Ndipo Yeye akasema, "Mimi ni Yesu."

15 Na sasa katika saa hizi za mwisho, kuiona Hiyo ikirudi kwetu. Basi usiku huo wakati Hiyo ilipopigwa picha rasmi huko Houston, Texas, ninii. . .Ndu—ndugu fulani, mhudumu wa Kibaptisti alikuwa akijadiliana na Daktari Bosworth, kama wengi wenu hapa labda walikuwako kule, kuhusu uponyaji wa

Kiungu, na mimi. . .kasema kwamba nilikuwa mponyaji wa Kiungu. Daktari Best alisema hivyo.

16 Ndipo nikasema, "Iwapo kuhubiri Injili ya wokovu, na kuamini ya kwamba Yesu huwaponya wagonjwa, kwa sababu kwamba Neno lilisema hivyo; kama hiyo ingenifanya mponyaji wa Kiungu, ingemfanya mtu anayeamini katika wokovu mwokozi wa Kiungu, kwa sababu ni Neno lile lile, mnaona." Yeye ni Yehova Yire na Yehova Rafi.

17 Majina Yake yote makuu ya ukombozi yaliwakilishwa katika Yesu Kristo, na hapo ndipo yalipotolewa na kuadhimisha kile Mungu alichokuwa. Ambapo, zile sifa kuu za Mungu kabla hata ya Yeye kuwa Mungu, kabla hapajakuwapo. . .Mungu ni kitu cha kuabudiwa. Kabla Yeye hajafanyika hicho, Yeye angali alikuwa ni Mungu. Yeye ni wa Milele, na sifa hizi zilikuwamo ndani Yake. Nazo zinajionyesha tu zenyewe, kama vile kuwa Baba, na Mwana, na—na Mwokozi, na Mponyaji. Hizo ni sifa tu za Mungu zikijionyesha zenyewe. Kwa hiyo tunashukuru ya kwamba tuna majaliwa ya kufurahia wakati huu mzuri wa ushirika na hakikisho la wokovu wetu, kupitia sifa za Mungu, Ambaye ndiye Mwokozi. Jina Lake na lisifiwe!

18 Sasa ninataka kumshukuru Ndugu Vayle, mtu hodari wa kuyaeleza mambo haya. Mimi si mwanatheolojia, kama mtu yeyote ajuavyo. Ni kwamba tu mimi sina elimu.

19 Nilimsikia maskini ndugu huyu hapa kutoka kwenye Moody Bible, akisimama, nami nikawazia, "Jamani, laiti ningalikuwa na elimu ya mvulana huyo." Nami ninatumaini ya kwamba Mungu, akimpa ono hili, atamtumia.

20 Kwa vile ninazeeka, ninapoendelea safarini, kwamba jamaa hawa wadogo watakuja na kuichukua Injili hii, kwa njia yenye nguvu zaidi kuliko ilivyo sasa. Wakati vizazi vinapoondoka, naye adui anaingia, Mungu anaendelea kuinua hali juu zaidi na zaidi na zaidi, mpaka hatimaye tutakutana na Kristo. Huyo Ndiye tunayetarajia kumwona, hata hivyo.

21 Sasa kumbukeni juma hili na kumalizia kwa ibada. Na kila mtu amekaribishwa, na hata madhehebu yote.

22 Sasa huenda nikasema hili wakati nikiwa na nafasi. Kamwe msifikiri moyoni mwenu kwamba ninawapinga hao watu. Ninawapenda watu hao. Ni mfumo wa dhehebu ndio unaouvunja ushirika. Hiyo ni. . .Ninaenda Afrika Kusini sasa, baada ya kualikwa tangu nilipokuwa huko wakati wa mwisho, kwa kuwa tuna matawi fulani ya Wafanyabiashara wa Full Gospel. Na mimi si mfuasi wa dhehebu lolote, hakuna chochote ila hili la Wafanyabiashara wa Full Gospel, na hata hivyo si dhehebu; na wakati litakapofanyika, basi, bila shaka, itanibidi kuliacha, maana mimi. . .ni dhehebu. Kiumbe ni sawa, bali si dhehebu. Kwa hiyo sisi. . .

23 Ma—makundi huko Afrika, kama kule upande wa mashariki, ni watu wanaozungumza Kiingereza, na—na Pentecostal Assemblies of God. Upande wa magharibi, ni Waafrikana, ambao ni Kaburu; na kutoka kwa Kaburu, Mdachi, nao wana kile wanachokiita A.F. ya M., ninii ya Afrika . . . Misheni za Kimitume za Afrika.

24 Na kuna sehemu mbili za hizo, vitengo viwili. Wanabatiza, ubatizo wa utatu, kwa . . . Moja lao hubatiza, nafikiri, mara tatu, kifudifudi; mara moja kwa ajili ya Baba, mara moja kwa ajili ya Mwana, na mara moja kwa ajili ya Roho Mtakatifu, wakimfanya miungu watatu badala ya Mmoja. Na hilo lingine hubatiza mara tatu, kinyumenyume, katika Jina la Baba, na moja katika Mwana, na katika Roho Mtakatifu; wakibatiza mara tatu mbalimbali, mara moja kwa ajili ya Baba, mara moja kwa ajili ya Mwana, na mara moja kwa ajili ya Roho Mtakatifu.

25 Mmoja wao anasema, "Mbona, tunabatizwa katika mauti Yake; na wakati Yeye alipokufa, aliinama mbele."

26 Huyo mwingine akasema, "Ni nani aliyepata kumzika mtu kifudifudi? Unamzika kichalichali." Kwa hiyo kuna mambo kama hayo.

27 Na kila mmoja wao huniandikia barua, na kutia sahihi hapa, "Ndugu Branham, Afrika inakuita. Njoo mara moja, lakini utafundisha fundisho hili tafadhali?" Vema, siwezi kwenda kule kwa kitu kama hicho. Mnaona? Sijawahi . . .

28 Niliwekwa wakfu mhudumu wa Baptisti ya Kimishenari. Nami nina heshima kubwa kwa ajili ya ndugu zangu wa Kibaptisti, na—na ninawapenda, bali kwa utaratibu na karama ambayo imetumwa, sio kwa Baptisti, sio kwa Presbiteri, bali kwa Kanisa. Inanibidi kusimama katikati yao, huru; sio huru kutokana nao, bali ndugu pamoja nao. Ninaamini, kama kile kisima cha tatu ambacho Yakobo alikichimba, kuna nafasi kwa ajili ya sisi wote. Nami ni—ninaamini hilo. Ipo nafasi kwenye Chemchemi, kwa ajili ya kila mmoja wetu, kwa—kwa yeyote atakaye.

29 Sasa ninao, bila shaka, vema, nisingetaka kuwaita "wapinzani," bali ninao watu wasioukubali Ujumbe. Na, mbona, jamani, siwezi kuwazia vibaya kuwahusu. Yesu alikuwa na jambo lilo hilo katika siku Yake, kila mtu mwingine analo. Na kila wakati, kuhusu Ujumbe wa Mungu, ulimwerngu haujawahi kupokea Huo. Bali hilo halisababishi chembe moja ya uchungu kumhusu mtu huyo, ama watu hao, au dhehebu hilo. Ingali vile vile tu. Ninashukuru sana kwa ajili ya hilo. Hilo ni moja ya mathibitisho ambayo ninajua kwamba nimepita kutoka mautini kuingia Uzimani; haidhuru ndugu hao wanafanya nini, ningali ninawapenda, mnaona. Moyoni mwangu, ninawapenda, mnaona, maana ni upendo ambao—ambao Mungu ameuweka

moyoni mwangu kwa ajili ya ndugu zangu. Na sasa Bwana abariki.

30 Na sasa kabla hatujaliendea Neno, nitaomba ra—rafiki yangu mpendwa, mhudumu kijana anayeketi hapa nje, ambaye—ambaye. . .Kwa namna fulani alikuwa na kinyongo. Na yeye na maskini mke wake walikuwa wakija nyumbani kwangu kila mara, naye angeketi hapo na asingezungumza. Na ange—angeuliza tu swali moja, "Ndugu Branham, unaonaje, Bwana ameniita kwenye huduma?" Nami niliona vipaji vya kijana huyu mwanamume, kutoka kwenye chuo kizuri cha Biblia, lakini alipungukiwa tu. Kama vile Musa na mafunzo yake yote, yeye. . .kile Musa alichopungukiwa nacho, kile kichaka kilichowaka moto kilikuwa nacho. Hicho ndicho Ndugu Ruddell alipungukiwa nacho, ni kile kichaka kilichowaka moto kilichokuwa nacho, na siku moja kikashika moto. Naye ndugu huyu ana kanisa kule nje kwenye vitongoji vya mji kabisa, ninaamini, wa Jeffersonville, kazi halisi inayoendelea kwa ajili ya Bwana, moja ya makanisa dada kutoka Maskanini.

31 Nami ningependa kama Ndugu Don Ruddell, ninamwona ameketi hapa nyuma, angesimama kwa miguu yake na kuomba dua, kusudi Roho Mtakatifu alitumie Neno, asubuhi ya leo, kwa njia ambayo angeona kulitumia. Ndugu Don, tafadhali, tunapoviinamisha vichwa vyetu.

[Ndugu Don Ruddell anaomba—Mh.] Naam, Bwana. Amina.

32 Hebu tugeuke sasa kwa ajili ya kusomwa kwa Maandiko, ninapobadilisha yale niliyokuwa ninaenda kusema asubuhi ya leo, niliyokuwa nayo niani kusema, baada ya kusikia kuhusu hii *Sauti* ya Wafanyabiashara. Mnajua, nimekuwa na wazo dogo kuhusu hili, mimi mwenyewe. Basi na tugeukie Marko Mtakatifu mlango wa 10, na tuanzie kwenye kifungu cha 17, ninaamini, ndivyo nilivyoliandika hili hapa chini.

> *Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, akaja. . . mbio, na* akipiga magoti *mbele yake, akamwuliza, Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?*
>
> *Yesu akamwambia, Kwa nini unaniita mwema? Hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu.*
>
> *Wazijua amri: Usizini, Usiue, Usiibe, Usishuhudie uongo, Usidanganye, Waheshimu baba yako na mama* yako.
>
> *Akajibu akamwambia, Mwalimu, haya yote nimeyashika tangu utoto wangu.*
>
> *Yesu akamkazia macho akampenda, akamwambia, Umepungukiwa na kitu kimoja, enenda,* na *uuze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na* hazina *mbinguni; kisha njoo, uchukue msalaba* wako, *unifuate.*

*Walakini yeye akakunja uso kwa neno* hili, *akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na* mali *nyingi*.

33 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno.

34 Nitakuwa nimekuwa na maskini, namna fulani ya msemo mdogo ambao mimi. . .karibu na Wafanyabiashara wa Full Gospel. Baadhi yao, kama sisi wahudumu tujuavyo, wangeniambia, "Aisee, wewe ni mhubiri, unafanya nini—unafanya nini karibu na hao wafanyabiashara?"

Nikasema, "Mimi ni mfanyabiashara."

Wakasema, "Uko kwenye biashara ya aina gani?"

35 Nami nikasema, "Hakikisho la Uzima wa Milele." Mnaona, sio bima, sasa. Hakikisho!

> Hakikisho lililobarikiwa, Yesu ni wangu!
> Loo, ni kionjo jinsi gani cha utukufu wa Kiungu!
> Mrithi wa wokovu, aliyenunuliwa na Mungu,
> Nimezawa kwa Roho Wake, nikaoshwa kwa Damu Yake.

36 Nami ningetaka kuninii, kwa kuwa hawa ni wafanyabiashara, nao wafanyabiashara hupenda kuzungumza kwa lugha ya biashara. Nami ninataka kuwaambia wanaume wafanyabiashara, na wafanyabiashara wanawake pia, wanaoketi hapa, ninataka kuchukua fungu hili, kwanza, na kuliita: *Uwekezaji*.

37 Sasa karibu kila mfanyabiashara anapenda uwekezaji mzuri, imara. Kama wewe ni mfanyabiashara, hiyo ni kusema, unavutiwa na hilo. Na nanii—na mfanyabiashara daima anatafuta uwekezaji mzuri, imara. Mnajua, ni—ni jambo zuri kwamba ndivyo tulivyo. Nami ninaenda kuzungumza nanyi asubuhi ya leo juu ya u—uwekezaji bora kuliko wote niujuao. Na ninawatakeni msikilize kwa makini, juu ya: *Uwekezaji*.

38 Sasa si—si sera nzuri hata kidogo kwa mfanyabiashara kubahatisha. Hata hivyo, kubahatisha ni kucheza kamari, na kucheza kamari ni kosa. Hatutaki kucheza kamari juu ya chochote, kwa sababu si—si sahihi. Baadhi ya hizi hapa, "lala maskini amka tajiri," mwajua, wakala fulani au kitu fulani ambacho hata hakijaimarishwa vizuri, lakini anaweza kuwasilisha jambo fulani kwako linalosikika ni zuri sana, ungesema, "Loo, jamani," na unaruka tu kuingia katika hilo. Na unapofanya hivyo, muda si muda wajua, unajikuta umefilisika. Bali kama mtu ni mfanyabiashara mzuri, mwenye akili, hana budi kwanza kujaribu kupata biashara ambayo imeimarika, shirika la zamani linaloaminika.

39 Na, halafu, si jambo jema kwa mfanyabiashara kuweka pesa zake mfukoni mwake. Kama huninii. . .Kama ukiweka fedha zako mfukoni mwako, hazitakuzalia chochote. Bali inakupasa

kuifanyiza kazi mahali fulani, kuitoa. Na, halafu, angalia unachofanya nayo.

40 Sasa, nafikiri kwa namna fulani hayo ni matamshi ya biashara, ambayo tungetumia. Nafikiri ni jambo la mantiki kwamba tunaliwazia jinsi hiyo, juu ya yale ninayoenda kusema. Sasa tunaona ya kwamba kama wewe. . .Tunao wengi sana ulimwenguni leo hii, ni njia za mkato, na "lala maskini amka tajiri," na wanatokea mara moja *hapa* na *pale*.

41 Na nilikuwa tu na rafiki ambaye alipoteza akiba ya maisha yake yote, kwenye ja—ja—jambo kama hilo, kwamba mtu fulani alimwambia, "Wekeza fedha zako *hapa*. *Hili* ndilo. *Hili* ndilo." Naye mtu huyo akaangalia hiyo picha iliyotiwa rangi iliyokuwa mbele zake, kisha akawekeza akiba ya maisha ya—yake katika hiyo, na akapoteza kila kitu alichokuwa nacho, ghafla, katika siku chache tu. Nayo kampuni hiyo ikafungwa, na hapo wakaondoka. Sasa, mwanadamu ni mjinga sana, kufanya ujanja kama huo. Mtu mzuri, mwenye akili timamu hatafanya biashara kwa masharti ya namna hiyo, mnaona.

42 Kwanza, inakupasa kuichunguza ka—ka—kampuni hiyo ambayo unaenda kuhusika nayo. Na ikiwa kampuni hiyo si nzuri, haijalishi wanakupa pendekezo zuri jinsi gani, hutafanya hivyo. Kama wewe ni mfanyabiashara mzuri, hutabahatisha namna hiyo, akiba yako ya maisha, kuwekeza katika kitu kama hicho.

43 Na sasa tukisema hayo, tukiyalinganisha, kuna mengi ya vitu hivi vya kidini ambavyo vimeinuka katika siku hii ya mwisho, ambayo ni ya "kufanyika ghafla." Na usiku wa leo wewe ni mwi—mwimbaji wa baa, na kesho unahubiri Injili. Mimi—mimi siendei upuuzi kama huo. Hasha. Nafikiri mtu anapaswa kuthibitishwa, kwanza.

44 Nafikiri hapo ndipo wengi wetu madhehebu ya Kipentekoste tulipolegeza kidogo hapo. Kwa sababu, tunamchukua mwanamke usiku wa leo, yeye ni mvua nguo juu ya—juu ya jukwaa mahali fulani, na usiku unaofuata yuko huku nje akiimba mahali fulani, na anatoka nje na anayo Biblia chini ya mkono wake, "Bwana alimwita kuhubiri." Sitilii hilo shaka. Hilo ni sawa, bali nafikiri mwanamke huyo anapaswa kuthibitishwa, kwanza. Hiyo ni kweli. Hebu ithibitishwe, hebu hiyo mbegu ikue kidogo, na tuone ni maisha ya aina gani yaliyoko nyuma yake.

45 Maana, hata watu atakaojihusisha nao hawataamini ushuhuda wa mwanamke huyo, wala ushuhuda wa mwanamume, yeyote yule, kama wakimwona mwanamke huyo usiku mmoja, ama mwanamume usiku mmoja, kwenye baa, na usiku unaofuata huko nje akiwa na Injili. Wanasema, "Ni udanganyifu wa—wa aina gani huu hata hivyo?" Bali wakati mwanamke huyo anapoishi maisha mazuri sana mjini,

kwa kitambo kidogo, na miongoni mwa watu, mpaka waone pana mabadiliko katika mwanamke huyo, basi ushuhuda wake utakuwa dhahiri. Mpaka wakati huo, ingekuwa heri aishi tu maisha, mpaka yaimarishwe.

46 Sasa, hatutaki hii "lala maskini amka tajiri." Ni...Pia hatutaki kuiweka, kwa sababu ukiweka pesa zako, nasema, "Wezi watavamia na kuziiba."

47 Na kama una jambo fulani moyoni mwako kwa ajili ya Mungu, na wewe hutalieleza, na kadhalika, na unaendelea tu kuliahirisha, "Vema, baadaye, baadaye." Basi maskini shauku hiyo uliyokuwa nayo wakati mmoja, kumtumikia Mungu, itaondolewa kwako. I—ibilisi ataingia na kuiba hiyo, na ndipo hutakuwa na shauku yoyote kumtumikia Yeye.

48 Kwa hiyo kama una shauku iliyo ndogo sana! Hapana shaka kuna kitu fulani ambacho hata kilikuleta kwenye kiamshakinywa hiki asubuhi ya leo. Kuna kitu. "Imani huja kwa kusikia, kulisikia Neno." Na lazima kuwe na shauku fulani la sivyo hata usingekuwako hapa. Sasa, usiachilie hiyo shauku itokomee kwenye maskini "jiunge," ama "peana mikono," au "nyunyiziwa," ama kitu fulani huko nje. Hebu tutafute kampuni halisi ambayo imeimarika, kitu ambacho—ambacho kwa kweli ni sawa.

49 Kampuni fulani ya kutegemewa ambayo hulipa kwa mgao mkubwa wa faida, hivyo ndivyo unavyotaka kuwekeza, ni kitu ambacho kinastahili.

50 Nami ninawazia, sababu ya mimi kuwazia hili asubuhi ya leo, ninaamini, kwa ajili ya kundi hili, ilikuwa ni huyu mtawala kijana tajiri, maskini kijana huyu kama tunavyomjua, anayeitwa mtawala tajiri. Alikuwa ni jamaa mdogo, hapana shaka, mtu mzuri. Alikuwa amekuzwa kwenye nyumba nzuri, labda katika nyumba ya kidini sana, kutokana na vile alivyomwendea Bwana Yesu.

Mwajua, Yesu alimwambia, "Zishike amri."

51 Naye akasema, "Hili nimefanya. Nimezishika hizi tangu utoto wangu. Nimefanya hili." Mnaona, yeye alikuwa na m—msingi mzuri. Hilo linamaanisha mengi sana, kwa maana kwa kawaida labda kamwe asingalimwendea Yesu.

52 Bali hapana shaka kulikuwako na jambo fulani kumhusu Yesu, ambalo lilivutia usikivu wake, tofauti na yale ambayo kwamba alikuwa amezoea katika sinagogi lake. Kwa sababu, unaona, Yesu alikuwa tofauti.

53 Na kama vile jamaa huyu mdogo ndiyo kwanza ashuhudie, kutoka kwenye—kwenye Chuo cha Biblia cha Moody hapa chini; mahali pazuri, hapana shaka hata kidogo. Lakini, unaona, siku moja alipata kitu fulani ambacho, unaona, kilikuwa tofauti, na yeye—yeye alipewa nafasi.

54 Basi huyu kijana mwanamume alipewa nafasi kwa ajili ya uwekezaji. Akiwa ni mfanyabiashara, jinsi alivyokuwa, mtawala, bila shaka, alikuwa na mali nyingi. Na Yesu alijua kulikuwako na uwezekano mkuu kwa huyu kijana mwanamume, kwa sababu Biblia ilisema, “Alipomtazama, Yeye alimpenda.” Hapana shaka alikuwa mtu mwe—mwema, mwenye tabia nzuri, na mwenendo wake ulikuwa ni wa kiungwana.

55 Kamwe hakukimbia kule na kusema, kama vile maskini Riki fulani wa siku hii angesema, “Aisee, Wewe! Njoo hapa, Hubiri!” Huo haukuwa ndio mwenendo wake.

56 Alikuja na yeye akasema, “Mwalimu mwema.” Mnaona? “Bwana, ama Mwalimu, nifanye nini ili nipate Uzima wa milele?” Sasa, unaona, alikuwa amepata, katika Yesu; ingawa alikuwa amezishika amri, ingawa alikuwa amekuwa mwaminifu kwa sinagogi lake na kwa huduma, bali hata hivyo alipata kitu fulani katika Yesu ambacho hicho kilitoa Uzima.

57 Sasa, torati haina Uzima ndani yake, hata kidogo. Ule Uzima. . .Torati, samahani, torati ni askari tu ambaye hukuelekeza kwenye dhambi zako, bali haina neema ya kuisamehe dhambi yako. Inakuelekeza tu na kukwambia kwamba wewe ni mwenye dhambi.

58 Na hilo limegeuzwa hata limeingizwa katika Ukristo, utaratibu tu, kusema tu kwamba inatupasa, na kufanya ma—ma—maazimio ya—ya kanuni za imani ama sheria, sheria ndogondogo za Ukristo. Na—nasi tumekuwa na uwezo sana, pamoja na wenye elimu, kuuwasilisha huu kwa ulimwengu. Bali, mnaona, hatuwaoni wakiuchukua kama inavyowapasa, kwa sababu hauna Uzima ndani yake. Mnaona, sisi, hatuna budi kutafuta kitu ambacho. . .Kila mtu anachungulia kupita pazia la kutoka hapo, mahali fulani huko ng’ambo, ambako alitoka, na anajua hana budi kurudi siku moja. Kila mtu anataka ku—kuona hilo, anataka kujua kile kilicho ng’ambo ya hapo.

59 Picha ya kupendeza sana. Yesu alisema, “Pepo mchafu anapomtoka mtu.” Hivi mliona kamwe Yeye hakusema, “Wakati ametolewa kwa mtu”? Bali wakati akiondoka kwa hiari yake mwenyewe, “Wakati pepo mchafu anapomtoka mtu, naye anarudi kwa mtu huyu na anakuta nyumba alimoishi imefagiliwa, ikapambwa, basi yeye huenda na kuwaleta ibilisi wengine saba, pepo, roho chafu, kisha wanaingia ndani ya mtu huyu, ndipo hali ya mwisho ya mtu huyu ni mbaya mara saba kuliko ilivyokuwa hapo mwanzo.” Mliona ya kwamba ibilisi huyo aliondoka kwa hiari yake mwenyewe, na akarudi kwa hiari yake mwenyewe? Sasa, kama nyumba hii ilikuwa tayari imekaliwa, wakati aliporudi, asingeweza kuingia ndani. Lakini, unaona, yeye aliipata tu imefagiliwa na kupambwa.

60 Ni picha nzuri sana ya mtu mwadilifu, kama tunavyoweza kuwazia leo hii juu ya mtu ambaye ni ninii—ninii. . .anajaribu

kuwazia kwamba anaenda Mbinguni kwa sababu tu kwamba ameachana na kucheza kamari, ama labda aliacha kutembea na yule mwanamke ambaye alikuwa si mke wake, ama aliacha unywaji wake pombe, kwenye Siku ya Mwaka Mpya, na akafungua ukurasa mpya na kujiunga na kanisa. Unaona? Unaona, haninii, yeye kwa kweli hajaongoka. Yeye tu ni mwadilifu. Na i—ibilisi anawatumia watu waadilifu ili tu ku—kuondoka na—na kufanya uwakilishi wa kijinga, wakati, kwa kweli, nguvu halisi za Kristo aliye hai hazimo mle. Mnaona, wao—wao . . .

61 Ulimwengu unataka kumwona Kristo. Yesu alisema, "Mimi ni Mzabibu, nyinyi ni matawi." Nalo tawi huushuhudia Mzabibu, kwa sababu hunyonya nguvu zake na Uhai kutoka kwenye Mzabibu. Vema, ule Mzabibu wa kwanza, tawi la kwanza lililotoka kwenye Mzabibu huu, hilo, waliandika Kitabu cha Matendo nyuma ya tawi hilo. Tunaona jinsi Roho Mtakatifu alivyotenda katika kanisa hilo la kwanza, lile kanisa la kipentekoste. Na ndipo wakati tu—tunapoamini ya kwamba kama Mzabibu huu asilia ukiwahi kutoa tawi jingine, wao wataandika Kitabu kingine cha Matendo nyuma yake, kwa sababu ni Uhai ule ule ulio ndani ya Mzabibu.

62 Na kama tawi la kwanza likitoa shada la zabibu, na halafu tuone kishada hapa nje kilicho na tikiti maji ikikulia juu yake, ama boga, au matango, tunajua ya kwamba huo sio u—uhai ulio kwenye mzabibu.

63 Kwa hiyo, nafikiri, hata mahali ambapo tungejiita wenyewe "Wapentekoste," tumeshindwa kuwakilisha kile—kile kitu halisi ambacho Kristo amekiweka tupate kukiwakilisha, Ro—Roho Mtakatifu na Uzima wa Roho. Mnaona, tunawakilisha wakati mwingine mihemko, na tunawakilisha furaha, lakini, na—na hilo ni zuri, bali kuna mengi kwake kuliko hayo. Lipo tunda linaloambatana nalo, ambalo mtu mwenye njaa analitafuta tunda hili la Roho, na hii ndiyo sifa iliyokuwamo ndani ya Yesu.

64 Kwa sababu, Yesu hakuwa tu mtu wa kawaida. Yesu alikuwa ni Mungu. Hakuwa kitu chochote pungufu ya Mungu. Sio tu nabii, hata ingawa alikuwa ni Nabii; Yeye alikuwa Mungu-Nabii. Yeye alikuwa ni nyu—nyumba ambamo Mungu wote aliishi. "Ndani Yake mlikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili."

65 Mungu akishuka kufanyika mtu, apate kufa. Mungu asingeweza kufa kama Roho, kwa sababu Yeye—Yeye asingeweza kufa. Yeye ni wa Milele, na asingeweza kufa. Lakini Mungu angeweza kujifanya Mwenyewe hivi kwamba angeweza kuhisi uchungu, na Yeye angeweza kuhisi na kuteseka. Mungu asingeweza kuteseka, kama Roho wa Milele. Bali alipofanyika Mwanadamu, Yeye angeweza kuteseka, na kuhisi u—uchungu na majaribu ambayo mwanadamu alipitia, kama vile Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni, na kila mtu tangu.

66 Ilibidi afanyike hilo, kusudi a—atimize sheria Yake Mwenyewe, kujitwalia juu Yake sheria Yake Mwenyewe. Asingaliweza kuwa ni mtu wa pili. Asingaliweza kuwa ni mtu wa tatu. Asingeweza kuwa kitu kingine chochote ila yule Mtu. Mnaona? Ilibidi awe.

67 Kama ningalikuwa na utawala wa ninii. . . kusanyiko hili, asubuhi ya leo, katika kiwango kile kile Yeye alicho nacho duniani, na ningesema, "Mtu yeyote akiiangalia ile nguzo, hana budi kufa." Na huyu kijana mwanamke Mkatoliki anayeketi hapa angeiangalia hiyo nguzo. Vema, ningesema, "Hata hivyo, yeye ni mgeni tu miongoni mwa hili, acha afe hicho kifo"? Lakini hata hivyo ni—ninaona huruma kwa ajili ya hu—huyu mama. Ningesema, "Basi acheni mtu huyu hapa afe mahali pake"? La, hilo lisingekuwa sahihi. Vema, ningesema, "Mwanangu, Billy Paul, nitamwacha Billy Paul afe mahali pake"? Hiyo bado si haki. Kwa sababu, mateso yako juu ya mtu mwingine, yakiniacha huru na hayo. Lakini njia pekee ninayoweza kuwa mwenye haki, kama Mungu alivyo mwenye haki, ingekuwa ni kuchukua mahali pake. Sina budi kuchukua mahali pake.

68 Kwa hiyo, ilibidi Mungu adhihirishwe katika mwili, apate kuona mauti, njia pekee Yeye angaliweza kufa, na kupitia hiyo Yeye akaleta ukombozi. Basi huyu kijana mwanamume aliona, ndani ya Yesu, kitu fulani zaidi ya kile amri zilikuwa nacho.

69 Sasa ninatambua hili, enyi waungwana, labda si katika imani tunayojaribu kuwakilisha, msininii. . . Sisi ni wawakilishi duni wa yale tunayojaribu kusema; ndivyo nilivyo mimi, mwenyewe, kwa kichwa kilichoinamishwa na moyo. U—Ujumbe ambao nimekabidhiwa kwa ajili ya kanisa katika siku hii, mimi ni mwakilishi duni wake. Na maisha yangu, ingawa ninajaribu kufanya yaliyo sahihi, ni—nina mema yangu na mabaya. Bali si—siwaombi mwangalie kile nilicho, kile nilicho. Tazameni kile ninachosema, Yule ninayezungumza habari zake, ni Bwana Yesu, ndani Yake kuna wokovu.

70 Basi jamaa huyu kijana aliona hilo, kwamba Mtu huyu hakika alikuwa na Mungu ndani Yake. A—angeweza kuangalia ndani ya mioyo ya watu na kuona shida iliyokuwepo, na angeweza kuwaambia juu yake; angewafufua wafu wakiisha kufa. Sasa, yeye alijua kwamba torati haikufanya kitu kama hicho, alijua kwamba kanisa lake mwenyewe halikufanya miujiza kama hiyo, hata hivyo alijua kwamba Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo, alikuwa yu hai; Yeye asingeweza kufa. Lakini aliona yote aliyokuwa Mungu, ndani ya Mtu huyu aliyeitwa Yesu, na moyo wake ukaona njaa.

71 Naye alijua hivyo, hata hivyo angekuwa mfuasi wa kanisa, mfuasi mzuri wa kanisa, labda baba yake alikuwa ni mmoja wa nanii wakuu, mdhamini, ama m—mmoja wa viongozi wakuu, ama kitu fulani kwenye halmashauri. Naye mvulana huyo

alikuwa amelelewa kwenye torati hiyo, naye alikuwa ameishika, kwa uchaji, na kuiheshimu. Hata hivyo, chini mle ndani, kuna kitu kilichotamani ku—kupata kitu fulani zaidi.

72 Ninatumaini ya kwamba hiyo iko moyoni mwa kila mwanamume na mwanamke hapa asubuhi ya leo, kupata kitu kilicho halisi. Kumbuka, huwezi kurudi na kufanya jaribio la pili. Inakubidi kulipata sasa. “Mti uegemeavyo, hivyo ndivyo uangukavyo.” Mimi . . .

73 Hakuna Maandiko kwa ajili ya toba ya baadaye. Hiyo ni kusema, huo ndio wakati wako sasa. Haidhuru jinsi linavyokuwa maarufu leo hii, na to—toharani mahali fulani, hakuna kama hicho, hakuna kitu kama hicho katika Biblia. Iliandikwa katika moja ya vitabu vya Makabayo, ama kitu kingine, bali hicho hakikuongezwa Kwake. Pia, angalia, katika kitabu hicho kimoja, toharani imetajwa, hata hivyo katika Biblia yote haijatajwa popote. Na, hata hivyo, Yesu akizungumza juu ya yuyu huyu kijana mwanamume wakati alipokufa, Yeye alisema, “Kuna shimo lililowekwa ambalo hapana mtu aliyewahi kuvuka, na kamwe hatalivuka, baada ya mauti.” Unaona? Na hilo latosha, wakati Yesu aliposema hivyo.

74 Sasa tunaona katika hili, ya kwamba njaa hii kwa ajili ya hili, kuwa m—mwenza, ama sio mwenza, bali cha—chanzo cha Uzima uliokuwa ndani ya Kristo, jamaa huyu mdogo alikuwa akitaka kuwa sehemu yake, kile tu Yesu alikuwa yuko pale kutoa, Kuzaliwa upya. Mnaona?

75 Hiyo ndiyo tuliyo nayo leo hii, nafasi ya kupokea Kuzaliwa upya, hata tunakuwa sehemu ya Mungu, mnaona, wana na binti za Mungu. Mnaelewa?

76 Angalieni, ni kama tu dhambi. Ka—kanisa kwa muda mrefu limesahau mahali pake; dhe—dhe—dhehebu, kwa kuliondokea Hili kipofu, kwa kipofu akimwongoza kipofu. Tazameni, kama ningalikuwa na tone moja la—la wino mweusi kwenye kalamu yangu hapa, na nilikuwa na kikombe hiki kimejaa sabuni, ama—ama beseni imewekwa hapa iliyojaa sabuni, ambayo wanawake hutumia. Sasa, ilikuwa kwamba sabuni . . .

77 Vema, nilipopata kitu kwenye shati langu, nilipokuwa mvulana mdogo tu, mama alikuwa anachukua mafuta ya makaa, ama terafini, ama—ama kitu fulani, na kuweka juu yake, na kujaribu kuondoa ra—ra—ra—rangi ya doa hilo. Aliitawanya tu, bali haikuwa yote mahali pamoja. Bali sasa wametengeneza kitu kinachoitwa sabuni. Na, jamani, sabuni hiyo itaondoa doa hilo sasa hivi.

78 Vema, kulikuwako na sheria ya Mungu, kwamba chini ya damu ya mwana-kondoo, hiyo haikuondoa dhambi, iliitawanya tu. Na wakati mwanadamu alipotenda dhambi, yeye alivuka hilo shimo kubwa, wakati alipotenda dhambi, akaondoka, alijitenga mbali na Mungu, pasipo kujiachia njia ya kurudi. Lakini Mungu,

katika rehema ya upendo, alikubali kibadala kwa ajili yake, na kibadala hiki kilidumu kwa maelfu ya miaka; bali kisingeweza kuondoa dhambi, kilifunika tu dhambi. Lakini wakati, sio kutengeneza . . .

79 Lakini Mungu, katika nguvu Zake za uumbaji, aliumba seli ya Damu, pasipo na tamaa ya kujuana kimwili, katika tumbo la uzazi la bikira; hiyo haifuniki tu dhambi, inaondoa dhambi. I—inaiondolea mbali sana hata haiko kwenye nia ya Mungu tena. Haitengenezi daraja ya kuvukia lile shimo, bali inaliondoa shimo hilo. Hiyo . . . Hebu mimina tone hili dogo la wino kwenye chupa ya sabuni, ama chochote kile, kamwe hutaipata hiyo rangi tena.

80 Hiyo rangi ilitoka wapi? Sasa, tunaona ya kwamba, katika kutengeneza rangi. Si—sijui. Mimi si mkemia. Ila ninasema tu, kama kungekuwako na mkemia anayeketi hapa, ungefikiri nilikuwa nimerukwa na akili, ama sikujua nilichokuwa nikizungumzia, kama nikitumia matamshi haya. Lakini kuwaacheni tu mjue kile ninachomaanisha, hebu tuseme sasa, hiyo rangi, sasa, mwanzoni, tungesema ilikuja, ni namna fulani ya asidi. Vema, basi, hiyo asidi ilitoka wapi? Hebu tuirudishe nyuma na kusema, vema, ilikuwa ni namna fulani ya asidi, ikaambatana na namna nyingine ya asidi, ipate kutengeneza rangi.

81 Ambapo, kuna rangi moja tu asilia, na hiyo ni nyeupe. Sote tunajua hilo, zingine ni upotovu kutoka kwake. Hakuna rangi ila nyeupe; hiyo ndiyo rangi halisi pekee iliyopo.

82 Sasa, sasa tunaona ya kwamba kemia hii, tutairudisha nyuma kwa muda kidogo tu, ndipo tunaona ya kwamba labda inasema inaishia sasa kwenye atomi. Vema, tungesema atomi B-moja mara atomi BC, mara nne, inafanyiza nyeusi. Kama ingalikuwa ni atomi B-nane, ingetokea waridi. Halafu molekuli mara molekuli mara *ninii* inatokea nyeusi.

83 Sasa hapo inaonyesha kulikuwako na akili fulani nyuma yake, iliyoifanya nyeusi. Halafu basi ukiipeleka mbele zaidi ya hapo, na mbele zaidi ya hapo, hiyo, mradi tu ni uumbaji, haina budi kutoka kwa muumba. Hapawezi kuwapo na kiumbe pasipokuwapo na muumba. Sasa tunaona basi wakati hii inapoingia, na rangi yoyote ni upotovu.

84 Na chochote nje ya mwana wa Mungu safi asiyeghoshiwa ni upotovu. Na dhambi ni kitu gani? Ni—ni haki iliyopotoshwa. Uzinzi ni kitu gani? Ni tendo ambalo Mungu alikusudia ili tu ku—kuijaza nchi, limepotoshwa. Ni kitu gani—uongo ni nini? Ni ukweli uliowakilishwa vibaya. Kwa hiyo, mnaona, kitu hicho chote sasa ni—ni upotovu.

85 Nayo rangi ya asili ni nyeupe. Inatupasa kuirudisha hii kuwa nyeupe, hata hivyo ni nyeusi. Imepotoshwa mahali fulani. Lakini wakati ikimiminwa katika hii, wino huu ukimiminiwa kwenye—

kwenye sabuni, inairudisha huko nyuma kabisa, na ni nyeupe tu kama ilivyo sabuni. Kamwe hutaipata tena. Imekwisha, milele.

86 Sasa, mihemko yenu yote, kama vile sisi Wapentekoste tunavyopenda kuruka na kupaza sauti. Mimi napenda. Ninaamini hilo ni sawa. Tunapenda kunena kwa lugha. Ninaamini hiyo ni karama ya Mungu. Ibilisi anaweza kuiga chochote unachoweza kutoa katika mkondo huo, bali angalia, basi inaonyesha kwamba kuna kasoro fulani, Uzima wa Kristo hautiririki kanisani jinsi unavyopaswa kufanya. Mwili, Bibi-arusi, haupitii mle ipasavyo. Sasa, unapata, umezibika mahali fulani.

87 Angalia, wakati hii, dhambi zako zinapoungamwa, nazo dhambi zako zinamiminiwa kwenye sabuni hiyo ya Damu ya Mwana wa Mungu, inaondolea dhambi mbali sana hata ina—inawekwa katika Bahari ya Usahaulifu wa Mungu, na haiwezi hata kukumbukwa machoni Pake tena. Ndipo nini, hiyo, hilo humfanya mtu nini? Mwana wa Mungu. Mungu kamwe hakukumbuki kuwa mwenye dhambi. Wewe ni mwana, wewe ni binti, hakuna kumbukumbu ya dhambi tena hata kidogo. Mungu huiweka katika Bahari ya Usahaulifu, sabuni. Bahari ya Usahaulifu ni Damu ya Kristo iliyomwagika kwa ajili yako. Na kwa hiyo, basi, wewe na Mungu, ni Baba na mwana, kwa neema ya Yesu Kristo; si kwa chochote ulichofanya, bali kwa neema Yake. Nyinyi ni wana na binti za Mungu, na mshiriki wa baraka Zake na wa nguvu Zake na wa Uzima Wake. Uzima Wake umo ndani yako, kwa kuwa wewe ni mwana wa Mungu. Loo, kama kanisa lingaliweza, tungeweza tu kuwakilisha hiyo!

88 Si ajabu Yesu alisema, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo." Mnaona? "Kazi nizifanyazo mimi," Yohana 14:12, "yeye aaminiye, aliyekiri na kuniamini Mimi, mnaona, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Kwa sababu, Mungu yumo ndani ya mwa—mwaminio kama tu alivyokuwa ndani ya Kristo. Sio katika utimilifu aliokuwamo ndani ya Kristo, bali Yeye yuko ndani yako kama tu Yeye alivyokuwa, kwa sababu wewe ni mwana wa Mungu kupitia Yesu Kristo.

89 Loo, jinsi kijana mwanamume huyu na maisha yake ya kikanisa angaliweza kuona ya kwamba hili lilikuwa ni jambo fulani katika Bwana Yesu. Naye alikabiliwa na shida hii, kumjia Yesu, hata hivyo ilikuwa ni kinyume na kanisa lake. Bali alikuwa na ujasiri, alikuwa na—alikuwa na kitu fulani ndani yake, kilichotaka kujua, njaa, ndipo akamjia Bwana Yesu.

90 Basi jamaa huyu mdogo, ninamwazia akipewa nafasi wakati huo kwa ajili ya uwekezaji huu, bali hakuvutiwa na uwekezaji wa namna hiyo. Ilikuwa ni sawa kama angaliweza kuendelea kuishi na marafiki zake, na kuendelea kuishi katika mambo

aliyokuwa akifanya, na kujihusisha kwake, na hata hivyo hakuwa tayari kujisalimisha.

91 Sasa hapo ndipo tunapopata shida kubwa leo hii, ni, kanisa linajua Maandiko. Hapa, taasisi hii ambayo jamaa huyu kijana hapa alikuwa ndio kwanza atokee, na hawa, ndugu huyu wa Kibaptisti anayeketi hapa, wanalijua Neno hilo. Wao—wao—wao ni wanafunzi wa Neno. Na hata hivyo ikiwa . . . Wao wanasema, "Vema, tunaliamini, tunalikubali."

92 Ni kama tu chupa ya dawa, tiba fulani. Mnaona, si kuponya maadili; inazalisha Maisha ya Kristo. Mnaona? Kama ukiichukua Injili, basi unakuwa sehemu ya Injili hiyo. Na kama ukifanyika sehemu yake, kama vile Petro, Yakobo, na Yohana, na hao wengine, walivyofanya kwenye Pentekoste, maisha yako ni Kitabu kingine cha Matendo kilicho hai. Hakuna njia nyingine kwake. Yesu alisema, katika Marko 16, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Bali watu watajifunza, na wanapitia kwenye seminari na shule, kujifunza hiyo, bali hawataki yoyote yake wenyewe, hata hivyo wanafikiri wanayo. Naam. Wanafikiri kwamba wanayo, bali matendo hunena kwa sauti kubwa kuliko maneno yote. Mnaona, maisha yako—yako yanathibitisha, chochote ulicho.

93 Basi jamaa huyu hakuvutiwa na kitu kama hicho. Ingawa uwekezaji huu mkuu haukuwa kitu fulani tu cha ghafla, haukuwa tu kitu ambacho Yesu alimwomba, "Njoo, uruke ndani yake." Yesu alikuwa amethibitishwa kwelikweli, Mwana wa Mungu.

94 Mtu angewezaje kwenda kaburini ambapo mtu aliyekufa alikuwa amelala, na kusema, "Lazaro, njoo huku," ambaye hakuwa ni Mungu?

95 Mtu angewezaje kusimama ndani ya meli, wakati pepo elfu kumi wa baharini waliapa wangemzamisha Yeye, Yeye na wanafunzi Wake, usiku huo, na angeweza kuweka mguu Wake kwenye demani ya merikebu, na kuangalia juu na kusema, "Amani, tulia," nao upepo na mawimbi yakamtii?

96 Mtu angewezaje kuangalia ndani ya moyo wa mwanadamu, na kusema, "Umefanya *hiki-na-hiki* na *hiki-na-hiki*"? Ilibidi iwe ni Mungu.

97 Ilithibitishwa kikamilifu. Na yeye hakuombwa tu awekeze katika kitu fulani, ambacho, wazo tu la—la uongo, ama dini fulani potovu. Ilitambulishwa kikamilifu, kile uwekezaji wake ulipaswa kuwa ndani yake.

98 Kama angalisema, "Sasa sijui kuhusu hili." Lakini, unaona, alimwita Yeye, "Mwalimu mwema." Naye alijua kulikuwako na jambo fulani, bali hata hivyo hakuwa tayari kuinywa hiyo dawa, kwa sababu Yesu alimwambia afanye jambo fulani.

99 Na hilo ndilo linalosababisha kizuizi miongoni mwa watu leo hii, ni kwamba wao. . . Wanaamini kuna Mungu. Hakuna mtu mwenye akili timamu ila ambaye anajua kuna Mungu, kwa sababu, kama hamtambui Mungu, Biblia inasema dhahiri kwamba hana akili timamu. Yeye ni mpumbavu, mnaona. Biblia ilisema, "Mpumbavu amesema moyoni mwake, 'Hakuna Mungu.'" Sasa, bali kama anaamini Mungu yupo, lakini hata hivyo hayuko tayari kujitenga mwenyewe kwa njia ile ile ambayo Yesu alikuwa akimwomba kijana huyu mwanamume, kijana mfanyabiashara, apate kuwekeza.

100 Yeye aliona kitu Fulani, ndani ya Yesu, ambacho watu wengine kamwe hawakuwa nacho. Aliona kulikuwako na kitu Fulani ambacho Yesu alikuwa nacho, ambacho hao makuhani hawakuwa nacho. Aliona kitu Fulani ambacho marabi, walimu, hakuna mmoja wao aliyekuwa na Hicho. Bali alikitambua Hicho katika Yesu, na kukitambua Hicho kwamba ni Mungu. Lakini aliwazia, "Vema, kama ninaweza kuingia, mbona, na isinibidi kufanya haya yote, nitaenda nitafute kujua." Lakini akakuta kwamba kuna Njia moja tu ya kuja.

101 Na hapo ndipo ulimwengu hauna budi kujifunza leo hii, na Kristo ndiye hiyo Njia; sio kanisa, sio uanachama, dhehebu, nzuri ziwezavyo kuwa, na mimi sina chochote dhidi yao kwa njia hiyo. Lakini hata hivyo huna budi kutambua kwamba ni Kristo, kule Kuzaliwa upya.

102 Wanaume, enyi wafanyabiashara wa jiji hili, si—siyahukumu makanisa yenu, mnapoketi hapa. Tunawathamini kuwa hapa. Lakini nina—ninajaribu ku—kuwauzia hakikisho, asubuhi ya leo. Sijaribu kuwauzieni; mimi ni mwakilishi wa hili, wa shirika hili, na ni—ni—ninataka kuwaambia ya kwamba hati hii ya mkataba ni bure. Mnaona? Nayo imeninii, imetambulishwa vizuri duniani leo hii, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kwa kazi Zake zile zile, ishara Zake zile zile, Injili Yake ile ile, Neno lile lile la Mungu. Yeye ametambulishwa kikamilifu kama ilivyokuwa wakati huo.

103 Sasa upo hapa asubuhi ya leo kwa ajili ya sababu fulani. Unaona? Kwa nini, upo hapa kwa nini hata hivyo? Kuna mdundo mdogo mle ndani unaokwambia. Sasa, sisemi uliache kanisa lako. Wewe nenda kwa kanisa lako ukiwa mtu bora zaidi kuliko ulivyokuwa ulipoliacha, nawe utakuwa nuru iliyowekwa juu ya kilima, taa iliyowashwa na haijafunikwa na kikapu. Utakuwa na Uzima wa Milele.

104 Sasa tunaona, inamrudisha mtu moja kwa moja mahali walipo wa—wa—watu leo hii. Bi—Biblia ilisema hapa. . . Ninayo Maandiko yaliyoandikwa hapa chini, ningependa kuyarejea. Yesu alisema, katika sura ya 3 ya Ufunuo, kwamba ka—kanisa la Laodikia, kanisa la Laodikia, ndilo wakati wa mwisho wa kanisa. Na sote tunaamini ya kwamba tunaishi katika wakati

wa mwisho, nao huu ndio wakati wa mwisho wa kanisa. Sasa linganisha wakati huu wa kanisa na huyo kijana mtawala tajiri. Walinganishe.

105 Sasa, hivi Yesu hakusema, "Kanisa la Laodikia lilikuwa ni tajiri, lina mali nyingi, halikuwa na haja ya kitu"? Si hiyo ndiyo hali ya kanisa leo hii? Na hata hivyo Kristo amejifunua Mwenyewe kupitia nyakati tatu za kanisa, kupitia Luther, kupitia Wesley, na kupitia wakati wa Kipentekoste; amejifunua Mwenyewe katika. . .katika Neno Lake, la kuhesabiwa haki, kutakaswa, na ubatizo wa Roho Mtakatifu (kule kurudishwa kwa karama), na sasa utambulisho Wake Mwenyewe miongoni mwao. Mnaona, kujaribu. . .Na wewe kijana tajiri mtawala, wafanyabiashara wa Chikago, asubuhi ya leo, mnaona?

106 Laodikia! Tunaona, nyakati zingine zote za kanisa, Yesu alikuwa angali kanisani. Lakini kwenye Wakati wa Laodikia, Yeye alikuwa nje, akibisha, akijaribu kuingia ndani. Nao huu ndio wakati ambapo dhihirisho la Kristo linakuja kikamilifu kabisa katika sura ya Kristo, ndani ya Kanisa Lake, hata makanisa (kama vile ndugu yule alivyosema muda mfupi uliopita) yanafunga mlango. Na hata hivyo Yeye amesimama kwa upendo, akibisha, "Mtu yeyote akiona njaa ama kuona kiu." [Ndugu Branham anagongagonga—Mh.] Je! mnaelewa? Sisi, mnatarajia mlango uliofungwa, ni Wakati wa Laodikia. Biblia ilisema ingekuwa hivyo.

107 Na sasa kama ninii yako—kama dhehebu lako limeufungia mlango Ujumbe kama huu, na Mjumbe kama huyu! Sio mimi; mimi ni ndugu yenu, mjoli pamoja nanyi. Bali Mjumbe ni Roho Mtakatifu akijidhihirisha Mwenyewe kupitia wanadamu, Kanisa ambalo Kristo alilitakasa kwa ajili ya kusudi lili hili.

108 Na sasa mmekabidhiwa nafasi kuwekeza katika Uzima huu wa Milele. Biashara yako huenda ikawa ni halali na kubwa, bali hakuna biashara yoyote iliyo kubwa zaidi kuliko kuokoa maisha yako mwenyewe. Unaona? Unayo nafasi.

109 Sasa kanisa lako huenda likamtoa Yeye nje, lakini, kwa jumla. Lakini Yesu hakuja tu kwa ajili ya kanisa fulani, kundi fulani tu. Yeye alikuja kwa ajili ya watu binafsi. "Mtampokea Roho Mtakatifu," mtu binafsi. Sasa hilo ndilo lililomleta.

110 Sasa tunaona ya kwamba Wakati wa Kanisa la Laodikia sasa umekabidhiwa nafasi ile ile ya uwekezaji katika Mtu yule yule ambaye yule kijana tajiri mtawala alimkataa katakata. Vivyo hivyo na Wakati wa Kanisa la Laodikia linakataa Hilo katakata, wanamtoa Yeye nje. Wanapenda. . .

111 Ni nini huyu kijana mtawala, ni nini—ni nini alichosema? "Aliondoka amehuzunika, kwa sababu kwamba alikuwa na mali nyingi." Ilikuwa—ilikuwa ni nafasi kubwa, hata hivyo alikuwa ni tajiri sana hata a—akajisikia kwamba ingeharibu mali yake.

112 Nashangaa kama umaarufu wa mtu kwenye Kiwanis ama—ama kwenye chama, ama labda umaarufu wake kanisani, hata kama mchungaji, ungekuwa ni mkubwa sana katika dhehebu hilo, hata ungeondoka kwenye nafasi ile ile, na kuikataa kwa madharau, kwa sababu inge—ingeuharibu urithi wako na kanisa. Nashangaa kama ninii wako—kama utumishi wako wa kanisa, hilo dhehebu, ni mkuu vya kutosha kwako, asubuhi ya leo, hata ungeachana na Hiyo, baadhi yenu wanaume mlio wafuasi wa makanisa, na mnaketi hapa asubuhi ya leo kama wafanyabiashara? Wazieni hilo.

113 Yule kijana tajiri mtawala alikabidhiwa hiyo, naye akaikataa, na Kristo anageuka na kusema wakati huu wa kanisa utafanya jambo lile lile katika siku za mwisho. Sasa, iko katika Chicago sasa, kwamba umekabiliwa kufanya uamuzi. Wakati unakwisha. Inakubidi kuufanya mara moja. Fanya uamuzi wako kwa ajili ya Kristo, kuzaliwa na Roho Wake.

114 Sasa, sasa tunaona ya kwamba huyu tajiri alifanya jambo hili kwa sababu kwamba aliupenda ulimwengu. Aliupenda ushirika wake pamoja na dhehebu lake kuliko alivyoupenda ushirika pamoja na Bwana Yesu.

115 Wengi wao asubuhi ya leo, wanasema, "Vema, ningehesabiwa mmoja wenu enyi Wapentekoste, ningehesabiwa kuwa mtakatifu anayejibingirisha, kama nilifanya jambo kama hilo."

116 Sasa, hazina yako iko wapi, hata hivyo? Je! iko kanisani mwako? Iko kwenye biashara yako? Ama, iko Mbinguni? "Kwani popote ilipo hazina yako, hapo ndipo moyo wako utakapokuwapo pia." Kwa hiyo kwa nini usifanye uwekezaji asubuhi ya leo, wa Uzima? Biashara yako itakuwa majivu siku moja.

117 Sijui, yule ndugu aliyetoa unabii, na hao ndugu, hasa, kuhusu mawimbi ya bahari, huenda huo ukawa hivyo. Bali ninasema jambo moja, ninajua hili, Biblia inasema kwamba dunia hii itateketea. Na Chikago haijawahi kuwa na moto kama inaoenda kuwa nao siku moja. Naye Mungu, Mungu mwenye haki, hawezi—hawezi kuacha Chikago iepuke ghadhabu ya Mungu.

118 Kama rafiki mmoja alivyoliweka wakati mmoja, kwamba Jack Moore alisema, "Kama Mungu akikiacha kizazi hiki kiepuke, kutokana na kuikataa Injili, na kwa kufanya mambo wanayofanya, na kuishi katika aina ya dhambi ambayo wanaishi ndani yake, utovu wa uadilifu na kadhalika, mbona, ingembidi Yeye kuinua Sodoma na Gomora na kuomba msamaha kwa kuwateketeza."

119 Kwa hiyo, wameikataa, wameipuuza Hiyo, na wamemtazama Kristo usoni. Hiyo, huduma ya Kristo, haijawahi kuwa kitu kikuu cha ulimwenguni kote. Ni unyenyekevu.

Mbona, Yeye alikuwa ulimwenguni katika siku za huduma Yake, labda theluthi moja ya Wayahudi huko Palestina kamwe hawakujua chochote juu Yake mpaka Yeye alipokuwa ameondoka. Mnaona? Mnaona? Na wao—wao kamwe hawajui mpaka imechelewa kupita kiasi.

120 Lakini hebu na tuwazie, asubuhi ya leo, kwamba hii ni siku maalum ambayo tumekabidhiwa, kama wafanyabiashara, kuwekeza katika Yesu Kristo; kusalimisha, kuwa tayari, na kuachana tu na kila kitu kilichopo, ambacho ni muhimu kwa ulimwengu huu, ili tuweze kupata hazina za Mbinguni. Kama Yesu alivyomwambia, "Kisha uje, unifuate Mimi, chukua msalaba wako."

121 Sio ukakuchukue umaarufu wako, ambapo kila mtu anasema, "Hakika, daktari, ingia moja kwa moja. Ni jambo kuu sana kuwa nawe hapa. Loo, shemasi, wewe nanii mzuri . . . "

122 Mnaona, ni msalaba. Na wewe, huenda wakakuita "mwendawazimu, uzushi." Na kama vile Paulo, ungeweza kushuhudia, "Katika njia iitwayo 'uzushi,' hiyo ndiyo njia ninayomwabudu Mungu wa baba zetu." Mnaona? Tumekuwa na watu wengine mbele zetu, ambao iliwabidi kufanya maamuzi haya.

123 Pia, kumbukeni, Mtakatifu Paulo na yule kijana mtawala wanatofautiana, Paulo alikuwa ni mtu mwenye nafasi kubwa mbele yake, pia, na alikabidhiwa hiyo, lakini aliikubali. Sasa unaweza kuangalia matokeo yao na ujiweke mwenyewe mahali, kile matokeo yako yatakachokuwa.

124 Unaweza kuliwekea msingi juu ya Neno, lisilobadili . . . lisilobadilika, hasa, Neno la Mungu, ahadi ya Mungu. Mungu hawezi kufanya jambo moja, kisha ageuke na kufanya jambo jingine tofauti kulihusu, na kusema ya kwamba Yeye alikosea mara ya kwanza. Mungu hawezi kubadilika. Yeye ni Mungu, na Mungu ni Neno.

125 Sasa Neno hili lilitambulishwa vizuri kwamba ni Mwana wa Mungu. Aliona kitu fulani ndani ya Yesu ambacho watu wengine hawakuwa nacho, ila gharama ilikuwa ni kubwa mno.

126 Nayo ni kubwa kupita kiasi leo hii, kwa kanisa la Laodikia. Lakini, kumbukeni, walitoka kwenye sinagogi kwa sababu kwamba, walimtoa Yeye kwenye sinagogi, kwa sababu hawakuwa na nafasi kwa ajili Yake katika sinagogi. Wanamtoa Kristo nje ya dhehebu leo hii, dhihirisho halisi lililo hai, lililotambulishwa kikamilifu, Neno la Mungu lililothibitishwa ambalo hakuna mtu anayeweza kulipinga, likithibitisha ya kwamba Kristo amefufuka katika wafu na Uzima Wake unaishi ndani ya watu Wake, akifanya jambo lile lile ambalo Yeye alifanya. Limefikia kuitwa "ibilisi, upiga ramli," na kila kitu kingine, lakini kumbukeni Neno ni lile lile. Neno moja dhidi

Yake halisameheki. Si katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao, hilo litawahi kusamehewa.

127 Huu ndio wakati wa mwisho wa kanisa. Isingeweza kuwa katika nyakati zingine. Ilibidi iwe katika wakati huu. Kila muda wa wakati, laiti tungalikuwa na wakati, ningejitolea kuweka hapa ndani na kuthibitisha hili. Neno la Mungu sasa linatimizwa. Nalo Neno la mwisho ambalo ninii. . .Kanisa lililoitwa litoke pamoja na Ibrahimu liko—liko katika mfano, na Sodoma. Sasa kumbukeni, Yeye—Yeye alielezea kinaganaga kabisa juu ya Sodoma. Mnaona? Sasa Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika Sodoma, katika siku za Lutu."

128 Mwangalie Billy Graham mamboleo, wale malaika, wajumbe huko chini Sodoma, wakiwaita hao watu wotoke, kuona kama wanaweza kupata watu arobaini wenye haki; na Mungu hata angepatana kwa watu kumi, na hata hivyo hawawezi kupata. Mwinjilisti huyu mashuhuri, Billy Graham, na Jack Shuler wa nyinyi watu wa Methodisti, na, loo, Oral Roberts wenu ninyi Wapentekoste, jinsi ambavyo huko nje katika Babeli katika madhehebu haya yanayoshirikiana.

129 Lakini, kumbukeni, Ibrahimu hakuwakilisha yoyote ya hayo; yeye hakuwa mji. Alikuwa akiutafuta Ufalme, a-ha, na alikuwa na kundi pamoja naye. Na kulikuwako na Mmoja wa wale watatu aliyebaki nyuma na kumwonyesha ishara kwamba Yeye alikuwa ni Nani, huku mgongo wake umeelekezwa kwenye hema, na kujua kile Sara alichosema ndani ya hema, utambuzi wa roho. Yesu akisema dhahiri, sasa kumbukeni hiyo ilikuwa. . .Hapakuwapo na ishara moja zaidi iliyofanywa mpaka Sodoma ilipoteketezwa. Jambo la mwisho ambalo Kanisa linaenda kuona, ni Kristo akidhihirishwa katika nguvu Zake, katika utimilifu, katika Kanisa Lake, kabla tu moto haujashuka. Kumbukeni, Lutu alikuwa ndiye yule ambaye moto ulianguka kutoka angani. Sio—sio huko nyuma katika siku za Nuhu; maji yalikuja. Bali Kristo alielezea ni huduma ya namna gani ingekuwako kwenye siku za Lutu, na sasa tunamwona Roho Mtakatifu akitenda kazi miongoni mwa Kanisa Lake, kwa njia ile ile. Tunaliona katika hali ya Laodikia, kama tu ilivyokuwa wakati ule.

130 Sasa hebu tuone hapa ni kwa nini mtu huyu asingewekeza kwenye hati hii ya mkataba, mmiliki wake, kwa sababu kwamba kulikuwa na mengi kupita kiasi upande ule mwingine ambayo hakutaka kuachilia.

131 Na hiyo ndiyo shida ya kanisa leo hii. Hakuna mtu aliye na akili timamu, papa, mtawala, au chochote kingine, anayeweza kusimama na kukana ya kwamba Yesu Kristo hakusema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Umbali gani? "Ulimwenguni kote, kwa kila kiumbe." Na hawezi kusema ya kwamba Yesu hakusema, "Kitambo kidogo, na

ulimwengu," kosmos, "utaratibu wa ulimwengu hautaniona Mimi tena." Utaratibu wa kanisa, utaratibu, utaratibu duniani, wa ulimwengu, wanadhani.

132 Na Ufalme wa Mungu kamwe si wa ulimwengu, haidhuru ni watu wangapi wenye elimu mnaoweza kusimama. Mimi siwahukumu hao watu, bali ninajaribu kuwaonyesha njama ambayo Shetani amefanya. Wao—wao hawawezi, sijali ni wakubwa jinsi gani. Nyinyi Wapentekoste mnataka . . . Nyinyi wa umoja mnataka wote wa utatu waungane na nyinyi. Nanyi wa utatu mnataka wote wa umoja na church of God, na kadhalika, waungane na madhehebu yenu thelathini na kitu, na kuwa moja. Nyinyi Methodisti na Baptisti, na kadhalika, vile vile.

133 Baraza hili la ekumeni ambalo linakutana tu kule juma hili, kujadili shi—shida, wote wanataka kuliunganisha liwe moja. Na watafanya hivyo. Biblia inasema watafanya hivyo, "Watafanya alama ya mnyama." Unaona ambapo msingi wenyewe unatokea? *Mnyama* ni "mamlaka," na itakuwa mamlaka, bali yatakuwa ni mamlaka mabaya.

134 Yesu alisema Ufalme Wake haukuwa ni wa ulimwengu huu. Kama ungalikuwa, Ufalme Wake, wajumbe Wake wangalifanya vita. Bali alisema, "Ufalme Wangu ni wa huko Juu." Mnaona? Ufalme wa Mungu sio dhehebu ambalo linaweza kuunda kitu kikubwa. Ni nguvu za Mungu, Roho Mtakatifu katika maisha ya binadamu.

135 Upesi sasa. Si—sitaki kuwaweka hapa muda mrefu, na tayari nimewaweka muda mrefu kupita kiasi sasa. Lakini je! ninaweza tu kuchukua dakika zingine chache? Naam, tutaharakisha. Nafikiri mnajua kile ninachozungumzia. Ni—nitaninii . . .

136 Hebu tuwachunguze tu baadhi ya wamiliki wa hati ya mkataba wa huu Uzima wa Milele, waliochukua uwekezaji huu katika Uzima wa Milele, wamiliki wa hati hii ya mkataba wa Neno la Mungu.

137 Kumbukeni, Hili ni Mungu katika herufi. "Maneno Yangu ni Roho," Yesu alisema. "Hayo ni Uzima." Je! Yeye alisema hilo? Yeye pia alisema hivi, katika Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, Biblia inatwambia, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa Mungu." "Naye Neno alifanyika mwili," kama ndiyo kwanza nimalize kuwaambia, "akakaa miongoni mwetu."

138 Yeye angali ni yule yule jana, Neno lililokuwako, Neno lililoko, na Neno litakalokuja. Yeye ni vitu vyote katika Biblia. Na kama ukiisoma Biblia na usimwone Yesu, basi afadhali urudi nyuma na kuyasoma Maandiko hayo tena. Kwa sababu, Huu ndio ushuhuda wa Yesu Kristo, Agano la Kale katika mfano, Agano Jipya likatimiza. Halafu, Yesu ni yule aliyekuwa, historia; Yeye aliyekuwa huko nyuma, mwanzoni. Unabii, Yeye alikuwa ndiye unabii. Alikuwa ndiye historia. Alikuwa ndiye Zaburi.

Alikuwa ni Bwana Yesu, na Yeye ndiye mambo yajayo, yaliyo katika Biblia. Kwa hiyo Yeye ni, Ushuhuda wa Yesu Kristo, ndiyo Biblia.

139 Sasa, na Biblia inaitwa Neno la Mungu, naye Mungu hana budi kuuhukumu ulimwengu kwa kigezo fulani. Kama Yeye akikuweka hapa pamoja na, na anaenda kukuhukumu, basi inabidi kuweko na kigezo fulani.

140 Unasema, "Kwa Yesu Kristo." Kila mtu ana wazo lake la Hilo.

141 Maskini mama huyu hapa, M—Mkatoliki. Asili yangu ilikuwa ni Katoliki, pia, unafahamu. Mimi ni Muairishi. Angalieni sasa, kanisa Katoliki linasema kwamba wao ndio kanisa. Sasa angalieni, kuna aina nyingi za kanisa Katoliki. Ni lipi kati ya makanisa ya Katoliki? Kama ni la Kirumi, basi la Orthodoksi ya Kiyunani limepotea. Basi kama ni la Orthodoksi ya Kiyunani, Warumi wamepotea. Kama ni la Kilutheri, basi Wamethodisti wamepotea. Kama ni—kama ni Methodisti, Wabaptisti wamepotea. Kama ni la Kipentekoste, basi hao wengine wamepotea. Bali kama ni Presbiteri, basi Wapentekoste wamepotea. Mnaona, linatatiza mno. Huwezi kulielewa. Ni lipi lililo sahihi? Hakuna hata moja la hayo lililo sahihi.

142 Yesu alisema, "Mimi ndimi Njia," na Yeye ni Neno, "Kweli, na Uzima." Hakuna mtu awezaye kuja, ila kwa Hiyo; si kupitia kanisa lako, kupitia kanuni yako ya imani, kupitia maombi yako. Inakubidi kuja kupitia Yesu! Yeye ni Mungu. Yeye ndiye Neno. Yeye ndiye Njia. Yeye ndiye Kweli. Yeye ndiye Uzima. Na kama taa imewekwa hapa isiyowashwa, nawe uiwashe taa, inatoa nuru. Itaakisi nini? Nuru ile ile iliyoakisi ilipowashwa kwa mara ya kwanza. Na wakati Injili imedhihirishwa, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Mnaliona?

143 Sasa hebu tuwachunguze tu baadhi ya wamiliki, sasa, na tuone kile kilichotokea katika siku yao mashuhuri ya kielimu. Kwa dakika zingine kumi ama kumi na tano tu, kisha tutafunga.

144 Nuhu aliwekeza katika ahadi ya Mungu, Neno la Mungu. Basi, kumbukeni, ilikuwa ni Neno la Mungu, ambalo Nuhu aliwekeza ndani Yake.

145 Na, hata hivyo, mara tu mtu anapowekeza, kumbukeni, Shetani atakuja hapo kuiondoa hati hiyo ya mkataba kutoka kwako, akiweza.

146 Imeandikwa, kwamba, "Mtu hataishi kwa mkate pekee," hayo ni maisha ya kimwili, "bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Sio tu sehemu Yake, kipande kidogo *hapa* na *pale*; bali "kwa kila Neno," mtu ataishi kwa Mkate wa Uzima. Basi Neno la Mungu ni nini? Ni Uzima, Roho, Uzima. Na wakati Hilo limedhihirishwa, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi

nizifanyazo naye pia atazifanya. Nyingi kuliko hizi atafanya, maana ninaenda kwa Baba."

147 Sasa, tunaona sasa kwamba Nuhu alijaribiwa wakati alipofanya uwekezaji wake.

148 Nawe pia, ndugu yangu. Na kama hakuna wakati wa majaribu, basi hujafanya uwekezaji wako bado. Kwa sababu, adui yako amesimama pale amevuta nyundo kwenye bunduki yake, huku upote umevutwa, naye yuko tayari kurusha kila mshale wa sumu awezao kurusha, kila dini potovu, na kila wazo dogo, na kila jitu la kielimu kama Goliathi. Yeye atawatuma huko, anayeonekana mrefu sana kuliko ndu—ndugu unaoshirikiana nao, maskini ndugu zako, wasio na elimu wala maarifa. Atatuma majitu wa elimu ya kiroho kama hao, na shule kubwakubwa, wanaoweza kuelezea na kuondolea mbali jambo hilo lote kutoka kwako. Lakini kama umefanya uwekezaji wako, na hati yako ya mkataba ikapigwa muhuri na kufungwa na Roho Mtakatifu, hakuna kitu kinachoenda kuifutilia mbali.

149 Hakuna mtu aliye na haki ya kuhubiri Injili mpaka kisiri, huko mbali upande wa nyuma ya jangwa, alisimama sakafuni yeye na Mungu peke yake. Hakuna mwenye elimu duniani angeweza kulielezea na kuliondoa kwako. Hiyo ni kweli, wewe ulikuwa pale, unajua lilitendeka. Haidhuru jinsi wanavyoweza kulielezea, "lakini, ngoja." Jambo fulani lilitukia, unajua lilitukia. Uliiona kwa macho yako. Ulizungumza na Hiyo; Hiyo ikakujibu, Nayo ikakutia muhuri ndani ya Utu Wake, nawe ukawa ni sehemu Yake. Utaondokea hilo jitu la kielimu. Na tuna wengi wa hao ulimwenguni leo hii, na wengine wa hatari, pia, ambao wamefunzwa vizuri kitheolojia, ama tukinena kitheolojia, wamefunzwa kutumia hayo, nao wanajua wanalofanya. Bali usiogope, Daudi, ikiwa Bwana Mungu yuko pamoja nawe.

150 Angalia, Shetani alimjaribu Nuhu, kwenye ninii yake—kwenye uwekezaji wake. Naye a—akamjaribu, kumfanya alitilie shaka. Wanasayansi waliinuka kumwambia hakuna mvua angani, na kulikuwako na wenye kudhihaki katika siku za Nuhu.

151 Sasa ikiwa kuna wenye kudhihaki katika siku hiyo, kwenye kuingia, kwenye wakati wa mwisho, hasa, juu ya uwekezaji ambao—ambao watu walichukulia moyoni mwao kuliamini Neno la Mungu, kuna wenye kudhihaki leo hii dhidi ya Neno, kwa sababu Hilo halionekani la kimantiki. Lakini, unaona, hupaswi kutumia akili yako mwenyewe.

Unasema, "Nilifikiri. Nafikiri. Mimi . . . "

152 Huna wazo lolote ama fikira inayokuja. Biblia ilisema, "Nia iliyokuwa ndani ya Kristo na iwe ndani yako." Na Yeye daima alifanya yale yaliyompendeza Baba, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno. Mnaona? Kwa hiyo hatuna wazo linalokuja. Inatubidi tu kuamini kile Yeye asemacho. Mimi sininii . . .

Sema, "Vema, siwezi kulieleza Hilo."

153 La, kama ungaliweza, basi ungaliweza kumweleza Mungu. Humjui Mungu kwa dhana ya kiakili. Unamjua Mungu kwa imani, ndiyo njia pekee unayojua jinsi ya kumwamini Mungu. Kwamba, huwezi tu kulieleza. Hakuna mtu anayeweza. Si juu yako kulieleza. La, hakuna mtu anayeweza kumweleza Mungu. Mungu haeleweki kwa maelezo; inakubidi kumwamini; isingekuwa ni imani tena. Sasa huna budi kuliamini. Sasa angalia.

154 Halafu, basi, uwekezaji mkubwa wa Nuhu siku moja ulileta faida. Wakati alipostahimili mateso, wakati alipowastahimili wenye kudhihaki, wakati aliposimama dhidi ya mambo yote na sera za ulimwengu wa siku hiyo, na mambo yote ya kidini yaliyoonekana kuwa dhidi yake, ililipa kwa kuokoa maisha yake. Aliliamini. Uwekezaji wake ukaleta faida.

155 Sasa, enyi wafanyabiashara, hebu niseme jambo jingine. Danieli aliwekeza siku moja. Alipelekwa chini katika ulimwengu ambao haukuwa kama ulimwengu aliouzoea. Alipelekwa miongoni mwa watu ambao hawakuamini kitu kile alichoamini. Lakini alifanya uwekezaji, basi angalia kile alichofanya. Alikusudia moyoni mwake kwamba asingeharibu, asingeuchafua uwekezaji huo. Unaona? Ule uwekezaji aliokuwa amefanya katika Mungu, alikusudia moyoni mwake; ingawa ilichukua maisha yake, yeye asingeuchafua kwa kutokuuamini.

156 Usikose kuuamini. Unapofanya uwekezaji wako, kaa hapo juu yake. Kama huko tayari kuuamini, basi usifanye uwekezaji wako. Lakini wakati ukiwa tayari kuacha nia iliyokuwa ndani ya Kristo kuwa ndani yako!

Unasema, "Vema, Hili ni *lile* na *lile*."

157 Afadhali ulichunguze. Kama haliko katika Neno, basi achana nalo. Neno ndilo mambo muhimu ya kimsingi na Kweli, hakuna tafsiri ya binafsi. Limeandikwa jinsi tu . . . Kama Mungu anaenda kulihukumu kanisa kwa Biblia, basi, Biblia, Mungu ameilinda Hiyo apate kuihifadhi, nayo imeandikwa jinsi tu Hiyo inavyopaswa kuandikwa. Hakuna tafsiri ya kibinafsi! Methodisti hulifasiri Hilo kwa njia moja, na Baptisti nyingine, na kadhalika. Na kisha kuileta kwenye mashindano ya kuamua, hakuna mmoja wao aliye sahihi. Ni akili ya mwanadamu, mahali wanapopotelea.

158 Kila wakati Mungu alipomwinua mwanzilishi mkuu kama Luther, na Wesley, na—na John Smith, na Calvin, Knox, Finney, Moody, ama kadhalika namna hiyo, halafu, baada ya kifo chao, basi waliunda dhehebu. Na kuwa na kundi la wa—waliohitimu chuoni wazuri hapa, waliweka tafsiri yao wenyewe Kwake na kuunda dhehebu, hapo ndipo ambapo walifia papo hapo. Na kamwe hakuna mahali, katika historia, ambapo kanisa lolote lililowahi kuunda dhehebu lilipata kuishi tangu hapo na

kuendelea. Ni wapi walipopata kuwa na miamsho mikubwa kanisani namna hiyo? Kanisa lilikufa wakati walipoliundia dhehebu.

159 Kutoka kwenye ka—kanisa Katoliki la Kirumi, kanisa la kwanza la Katoliki ya Kirumi kabla halijafanyika kanisa la Kirumi, lilikuwa ni kanisa katoliki kwenye Pentekoste. Karibu miaka mia tatu baadaye, huko Nikea, Rumi, likabadilika kutoka kanisa katoliki la kimitume likawa kanisa Katoliki la Kirumi, lililoingiza mawazo ya wanadamu, maskini ushirikina wa upagani wa Kirumi kwenye Maandiko. Na tangu wakati huo, kamwe halijafanya lolote ila kukaa pale, limekufa, likiwa na wafuasi.

160 Akatokea mtengenezaji, akaja Luther, naye Luther akatokea kama mtu wa Mungu, juu ya kuhesabiwa haki; Neno lilifundisha hilo, kwa neema ya Mungu. Ambapo, kanisa Katoliki lilisema, "Hakuna, hakuna wokovu nje ya kanisa. Mungu alikuwa katika kanisa Lake. Bi-. . . "

161 Nilikuwa kwenye mahojiano pamoja na kasisi, si muda mrefu uliopita. Akasema, "Bw. Branham, unajaribu kuzungumza kuhusu Biblia. Hili ndilo kanisa!" Kasema, "Mungu yuko ndani ya kanisa Lake."

Nikasema, "Nionyeshe ni wapi."

162 Biblia ilisema ya kwamba Mungu yuko ndani ya Neno. Yeye ni Neno. Na kama Neno liko ndani yako, Hilo linamzaa Mungu tena. Pia Yeye alisema, "Neno ni mbegu, nayo mbegu huzaa kile ya jinsi yake kilicho." Litazaa maisha ya kitauwa, maisha makamilifu yaliyowekwa wakfu kwa Yesu Kristo.

163 Sasa mwangalie Danieli, baada ya uwekezaji wake alioufanya katika Mungu, basi ulilipa kwa kuyaokoa maisha yake kutokana na tundu la simba.

164 Wana wa Kiebrania walifanya uwekezaji siku moja, hata wakati yale matangazo yalipotokea kwamba wote walikuwa wanaenda kulazimika kujiunga na kundi hili na kuabudu kwa njia nyingine mbali na njia ambayo Mungu alikuwa amewaambia ilikuwa ndiyo njia sahihi, walifanya uwekezaji katika Mungu. "Ingawa watatutupa kwenye tanuru, hatutafanya jambo hilo. Tutadumu pamoja na Neno hili." Uliyaokoa maisha yao, ukaliongoa taifa, mnaona, kwa sababu walikuwa tayari kudumisha uwekezaji wao. Naam, bwana.

165 Petro, mvuvi, alikuwa ni mfanyabiashara. Alikuwa na biashara kubwa. Aliuza samaki. Na hilo lilikuwa ni jambo kubwa katika siku hizo, akiishi pale karibu na ziwa, kama mahali kitu kama Chicago hapa, karibu na ziwa. Naye alikuwa mvuvi wa biashara. Lakini, naye kwa namna fulani alikuwa ni mtu mgumu, kwa sababu alikuwa ni Mfarisayo, na baba yake alikuwa mzee Mfarisayo. Lakini siku moja . . .

166 Ni—nilikuwa nikisoma hadithi. Na ingawa huenda isiwe ni ya kweli, na mimi . . . Labda si ya kweli, bali nafikiri ingestahimili jaribio sasa hivi.

167 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] " . . . kuja. Bali unajua, mwanangu, Yeye hajaja bado, na Yeye huenda akaja katika siku yako. Sasa kumbuka tu, kama baba yako, ninataka kusema jambo hili, ya kwamba kutakuwako na madhehebu mengi yatakayoinuka, kutakuwako na manabii wengi wa uongo watakaotokea." Kama Yesu alivyosema kuhusu siku hii. "Bali kwa tunda lao," nalo *tunda* ni tunda la Roho, unaona, "mtawatambua." Akasema, "Kutakuwako na wengi wa hawa," ambao walikuwako. Bali akasema, "Sasa nataka ujue huenda wakatokea walimu mashuhuri, wenye akili."

168 Ambao, kulikuwako na mmoja aliyedai kuwa ni Kristo, na akawaongoza mia nne wakatoka, nao wakaangamia nyikani, kwa sababu ilikuwa ni kinyume na Neno.

169 Akasema, "Lakini ninakutaka ukumbuke kwamba, Masihi huyu, Yeye atakuwa na kibandiko cha utambulisho juu Yake, na Yeye atakuwa ni Nabii. Sasa, sisi ni Waebrania, na Bwana Mungu ametwambia ya kwamba sisi . . . Yeye alitutumia manabii kwa sababu Neno la Bwana huja tu kwa nabii. Hiyo ni kweli. Na Yeye akasema, 'Akiwepo mmoja miongoni mwenu, aliye wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana nitasema naye. Na kile asemacho, kama kikitimia, basi msikieni. Lakini, kisipotimia, msimsikie, msimwogope mtu huyo. Lakini mwogopeni kama nyinyi . . . kama kikitimia, kile asemacho.' Ndipo Musa akasema, 'Bwana Mungu wenu atamwinua Nabii mithili yangu, naye Huyo mtamsikia.' Sasa, Masihi huyu atakuwa ni Nabii. Kumbuka, sio mwelimishaji, sio kuhani, sio kasisi, bali Yeye atakuwa ni Nabii."

170 Basi wakati Simoni alipoketi juu ya kipande hicho cha mbao, labda ile siku ambayo Andrea alimpeleka ufukoni mwa bahari. Ambapo Yesu . . . Baada ya wao kufanya kazi usiku kucha wasione kitu nyavuni mwao, wakaketi pale chini. Ndipo akaazima mtumbwi kutoka kwa huyu Petro. Na—na ndipo Yeye akasema, akiisha kumaliza kuutumia huo mtumbwi . . . Huenda Petro alisikiliza mazungumzo Yake, na labda akaweka vidole vyake nusu kwenye masikio yake, huku ameketi kwenye kipande hiki huko nje, wakati Yesu akielea pale, huko nje kwenye mtumbwi wake, kwa sababu ya umati.

171 Basi tunaona, kwamba, huko nje kwenye mtumbwi, hapana budi Yesu alimwashiria Si—Simoni, a—a—aulete mtumbwi. Basi alipoenda huko nje na kusema, "Sasa, najua mmefanya kazi usiku kucha, wala hamkupata kitu, bali kuna samaki upande *huu* sasa. Tupeni wavu wenu ndani, na kuna samaki wengi wanaongojea."

172 Vema, lingali ni neno tu. Lakini wakati alipoutupa wavu ndani na akaanza kuvuta, na kulikuwako na samaki, ambalo

pia lilimaanisha huyo hapo Masihi ambaye baba yake alikuwa amemwambia kumhusu, Nabii. Naye akasema, "Ondoka kwangu, Bwana, mimi ni mtu mwenye dhambi."

173 Akasema, "Usiogope, Simoni, sasa umeiona ile Kweli. Tangu sasa utakuwa mvuvi wa watu."

174 Petro alikuwa tayari kuziacha nyavu zake za kuvua samaki, biashara yake. Alifanya uwekezaji mkamilifu katika Yesu Kristo, kwa sababu aliona ya kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi aliyeahidiwa, kwa kuwa hilo hapo Neno alilonena likidhihirishwa, na huyo alikuwa ndiye Masihi. Alijua hilo ndilo ambalo Neno lilisema, ambalo baba yake mzee Mfarisayo alikuwa amemwambia, ya kwamba, "Masihi atakuwa Neno lililofanyika mwili, na Yeye atakuwa ni Nabii akiifanya ahadi hii ya Masihi kutimia," na ilikuwa ndiyo hiyo hapo. Kwa hiyo, Petro alifanya uwekezaji wake baada ya kuona utambulisho, thibitisho la Neno.

175 Nathanaeli aliwekeza, kama nilivyozungumzia jana usiku. Na vivyo hivyo yule mwanamke kisimani.

176 Nikodemo, mwanatheolojia mashuhuri, tuseme, kitu kama mtu fulani aliyenena asubuhi ya leo, mwanachuoni hodari. Na wao—wao walikuja, alikuja kuwekeza. Nami nawatakeni muone matamshi ya mtu huyu mashuhuri, Nikodemo, anayepatikana katika Yohana Mtakatifu mlango wa 3. Yeye hakuwa tu mtu ovyo ovyo. Alikuwa ni mwanatheolojia. Angalia kile alichosema.

177 Hapana shaka, Halmashauri ya Sanhedrin, taasisi, walikuwa wameijadili huduma ya Mtu huyu. Ingawa aliitwa Nabii wa Galilaya, hata hivyo kulikuwako na uchunguzi mkubwa uliofanyiwa huduma Yake.

178 Sasa angalia maungamo hayo, kama hayapiti juu ya kichwa chako. Angalieni kile Nikodemo alichomwambia Yesu. "Mwalimu! Sisi, Mafarisayo, tunajua. Hatuwezi kulikiri. Hatuwezi kulitangaza, maana tutapoteza wadhifa wetu. Sisi, tutapoteza uwekezaji wetu katika mkate we—we—wetu na siagi yetu. Tuta—tutapoteza wadhifa wetu miongoni mwa watu. Tutatengwa na jamii, kama wale Wagalilaya ama wavuvi. Tutahesabiwa mtu m—m—mbaya sana mwenye elimu, labda mwenye wasiwasi, fadhaa, mpagao, sio mtu wa kufanya uamuzi mzuri, kwa hiyo kanisa haliwezi kututumia tena kama tukifanya uamuzi huu. Lakini, lakini tunajua ya kwamba Wewe ni mwalimu aliyetoka kwa Mungu, kwa kuwa hakuna mtu awezaye kufanya mambo hayo unayofanya Wewe isipokuwa Mungu awe pamoja naye."

179 Mnaona, Nikodemo, wengi wetu wanaendelea sana kumhusu Nikodemo. Wanasema, "Alikuja usiku."

180 Alikuja kufanya uwekezaji wake, na akakuta benki ilikuwa imefunguliwa saa ishirini na nne kwa siku. Ingawa ni usiku, be—benki ilikuwa imefunguliwa. Imefunguliwa asubuhi ya leo,

hapa Chikago. Imefunguliwa wakati wote, kama uko tayari kuwekeza. Alikuta milango imefunguliwa, moyo mkaribishi wa kumpokea. Akampeleka juu ya nyumba, na wakati wameketi pale kwenye mwanga wa mwezi, ndipo basi Nikodemo alikuwa anaenda kufanya uwekezaji wake.

181 Basi akafanya maungamo yake kwanza, "Sisi tunajua kwamba Wewe ni mwalimu aliyetoka kwa Mungu, maana hakuna mtu awezaye kufanya mambo ufanyayo Wewe Mungu asipokuwa pamoja naye. Tunajua hilo." Sasa, a—alisema "sisi," hilo lilimaanisha lile baraza, mu—muungano wa baraza. Walikuwa na baraza la muungano, kama tunalojaribu kuingiza katika makanisa yetu, muungano wa makanisa, mnaona, Baraza la Ulimwengu. Basi akasema, "Sisi, tunafahamu hilo." Bali hakuna mmoja wa hao wengine aliyetaka kuvutiwa. Kama yule tajiri, walitaka kudumisha utajiri wao wa kilimwengu.

182 Rafiki yangu wa biashara, asubuhi ya leo, wanaume ama wanawake, ungeweza kudiriki? Hesabu gharama. Hivi itakuharibu sana kuukubali ubatizo wa Roho Mtakatifu? Hivi itaiharibu sana biashara yako? Ingekuwa heri kwako biashara yako iharibike hapa duniani, ama wadhifa wako kanisani ubadilishwe, ama ingekuwa heri kwako kuwa na Uzima wa Milele? Inategemea ni hati gani ya mkataba unayotaka kushikilia. Kumbukeni, Nikodemo alikuwa mtu mashuhuri, naye alikuwa na mambo mengi ya kuenda kinyume chake, bali aliikubali hati hii ya mkataba.

183 Tunaona katika Luka 24:49, kwamba, hawa wamiliki wa hati ya mkataba. Nami ninafunga katika dakika moja. Hawa wamiliki wa hati ya mkataba, katika Luka 24:49, wote waliokuwa wamefanya uwekezaji. Mwajua, kama ukiwa na hati ya mkataba, hulipa katika mgawo wa faida. Mara nyingi, ungeweza kupata mgawo wa faida kutoka kwenye hati yako ya mkataba. Vema, walikuwa wamemwamini Bwana Yesu Kristo, na walikuwa wamemkubali Yeye kama Mwokozi binafsi, bali wanafahamu kwamba kulikuwako na mgawo wa faida tayari kulipwa kwenye hati hiyo ya mkataba, kwani Yesu aliwaambia, katika Luka 24:49, "Tazama, natuma mgawo wa faida ulioahidiwa, ahadi ya Baba Yangu, juu yenu."

184 Yoeli 2:28 na Maandiko mengine mengi yaliyokuwa yameahidi hiyo. Ninaamini, Isaya 28:19, ambapo lilisema, "Amri lazima iwe juu ya amri, na kanuni juu ya kanuni; hapa kidogo, na pale kidogo." "Shikilia sana yaliyo mema." "Kwa kuwa kwa midomo migeni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa." Yoeli alisema, katika Yoeli 2:28, "Na itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili. Wana wenu na binti zenu watatabiri, na juu ya watumishi Wangu wanaume na watumishi wanawake nitaimwaga Roho Yangu. Na wana wenu wataona maono. Wazee wenu wataota ndoto. Na itakuwa kwamba kila

mmoja akayeliitia Jina la Bwana ataokolewa." Nao watu hawa wakaelewa, kwa Maandiko na kwa kumkubali Yesu Kristo kama hati yao ya mkataba wa Uzima, kwamba kulikuwako na mgawo wa faida.

185 Sasa, ewe mfanyabiashara, huenda ukawa mshiriki wa dhehebu fulani. Bali kuna mgawo wa faida. Huenda umemkubali Kristo, huenda umebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kama ubatizo wa Kikristo, huenda umefanya mambo haya yote, lakini hata hivyo kuna mgawo wa faida kwenye uwekezaji huu.

186 Na katika Luka 24:49, kama ndiyo kwanza niseme, wao—wao walipanda wakaenda kuchukua mgawo wa faida, na hapo wote walipokuwa wamekusanyika pamoja na kuanza kumngojea Bwana. Walingojea, sio tu kwa siku mbili au siku tatu.

187 Ndipo labda mtu fulani alisimama, labda tuseme ni Mathayo. Yeye alikuwa mtoza ushuru wa serikali. Huenda alikuwa ni mtu mwenye akili sana. Huenda alisimama na kusema, "Ngojeni kidogo! Kwa nini tungoje muda mwingine zaidi? Yeye alitwambia tupande tuje huku juu; sisi hapa. Sisi, tayari tumekuwa hapa siku nane sasa, nafikiri tunapaswa kuzitwaa huduma zetu na kuendelea." Bali hivyo sivyo Neno lilivyosema.

188 "Kwa midomo migeni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa." "Nitaimwaga Roho Yangu, na Mimi nitaonyesha ishara na maajabu." Walingojea thibitisho la ushahidi kwamba hati yao ya mkataba ilikuwa ni nzuri.

189 Nikizungumza na ndugu mzuri wa Kibaptisti, si muda mrefu uliopita. Sitalitaja jina lake, kwa sababu ni mtu anayejulikana sana, mtu mzuri kutoka kwenye kanisa kubwa. Yeye alinijia, na akasema, "Billy, kwa nini unajichanganyisha katika upuuzi kama huo?"

190 Nikasema, "Upuuzi gani?" Nikasema, "Nilichanganyikana ndani ya Kristo," kisha nikasema, "Uzima wangu."

191 Akasema, "Sasa wewe, uliyekuwa Baptisti hapo awali, unajua." Kasema, "Angalia, Biblia ilisema, 'Ibrahimu alimwamini Mungu, na ilihesabiwa kwake kuwa jambo la haki.'"

Nikasema, "Hiyo ni kweli."

192 Kasema, "Ni nini zaidi ambacho Mungu. . .ama Ibrahimu angefanya ila kumwamini Mungu?" Na yeye. . .

Nikasema, "Vema, wewe unamwamini?"

Akasema, "Naam, ninamwamini Mungu."

193 Ndipo nikasema, "Unafikiri basi," mimi nikijua fundisho la Kibaptisti, nikasema, "hivi unaamini kwamba ulimpokea Roho Mtakatifu?"

194 Akasema, “Bila shaka. Nilipoamini Hilo, nilimpokea Huyo, maana hiyo ndiyo sababu ya mimi kuamini Hilo.”

Nikasema, “Jinsi ilivyo kinyume na Mtakatifu Paulo, katika Matendo 19!”

195 Wakati alipokutana na wale Wabaptisti kule juu, ambao walikuwa ni waongofu wa Yohana kwa Kristo, yeye alisema, “Je! mmempokea Roho Mtakatifu, mkapata mgawo wenu wa faida, tangu mlipoamini?” Sio *wakati* mlipoamini, bali, “baada ya ninyi kuamini.”

Wakasema, “Hatujui kama kuna yeyote.”

Akasema, “Mlibatizwa namna gani?”

196 Kwa hiyo wakasema, “Tumebatizwa kwa Yohana, hilo linapaswa kulitatua.”

197 Yeye akasema, “Hapana, sio sasa. Yohana alibatiza kwa toba tu, si kwa ondoleo la dhambi; Dhabihu haikuwa imetolewa.”

198 Basi waliposikia haya, walibatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo. Paulo aliweka mikono yake juu yao, ndipo Roho Mtakatifu akaja juu yao, nao wakatabiri na kunena kwa lugha, nao wakapata mgawo wa faida kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

199 Akasema, “Mbona, Ibrahimu alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kwake.” Kasema, “Mtu anaweza kufanya zaidi kiasi gani?”

200 Nikasema, “Kwa kweli, yeye alimwamini Mungu, bali Mungu alilithibitisha kwa kumpa muhuri wa tohara. Na sasa wakati unaposema wewe ni ‘mwaminio,’ Mungu kamwe hajaitambua imani yako mpaka Yeye anapoitia muhuri kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu na Yeye ameitambua kama mbegu iliyokusudiwa tangu zamani.” Hilo lilikuwa ni neno zuri kwa Mbaptisti, mnaona. Mnaona? Na ni kweli. Hakika, ni kweli.

201 “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu isipokuwa Baba yangu amvute. Na wote alionipa Baba watakuja.” Ni jukumu letu kulihubiri Neno mpaka litoke nje. Zingine huanguka kando ya barabara. Lakini zingine huigusa mbegu hiyo huko ng’ambo na kuleta Uzima mara moja, wanaliona Hilo sasa hivi.

Kwa hiyo unaona, walienda na kuchukua mgao wa faida.

202 Naam, kijana tajiri Paulo aliliona thibitisho hili, kwa Roho yule yule, na Yeye akambadilisha wakati akiwa njiani kwenda Dameski. Kwa nini? Aliiona ile Nguzo ya Moto, naye akajua hiyo ilikuwa ni Yesu yeye yule. Ndipo akalia kwa sauti kuu, akiisha kujua ilikuwa ni Mungu. Na Yesu ni Mungu. Ndipo wakati Paulo angeweza kuona . . .

203 Akiwa ni mwanatheolojia, Paulo alikuwa na makusudio makuu. Alikuwa ni mwanatheolojia. Alifunzwa chini ya Gamalieli, yule mtu mashuhuri. Alikuwa na shauku za kuwa kuhani siku moja, ama—ama labda kuhani mkuu. Alikuwa ni

mwenye akili nyingi, msomi, mtu mashuhuri, kweli. Lakini wakati . . . Na hizi dini potovu, za kurukaruka na kukimbia huku na huku, na kufanya yasiyofaa kama walivyokuwa, alidhani walikuwa ni kundi la—la wazushi. Lakini alipokuwa njiani mwake kuenda huko Dameski, kama nilivyosema . . . Na, sasa, alikuwa tajiri, pia. Alikuwa ni mtu mzuri, kijana mwanamume, akiteremka barabarani, vipaji vyote alivyokuwa ameelimishwa, viliwekwa mbele zake, zile nafasi. Angalia tofauti kati ya yule mfanyabiashara tajiri na huyu mfanyabiashara tajiri; mmoja aliikubali Hiyo, na mwingine akaikataa Hiyo. Angalieni.

204 Halafu basi, mara ghafla, alibwagwa chini na Nuru, Nguzo ya Moto iliyosimama pale, naye akaitambua Hiyo. Akasema, "Bwana, U Nani Wewe?"

Na Yeye akasema, "Mimi ni Yesu."

205 Na wakati alipopata ufunuo kwamba Mungu na Kristo hawakuwa watu wawili tofauti, walikuwa ni Mtu yule yule, basi alikuwa tayari kuwekeza. Nashangaa kama tungeweza kuliona jambo lilo hilo leo hii. Wakati Paulo alipoona basi, akiwa ni Myahudi, kwamba, "Mungu yeye yule aliyeniongoza kupitia, aliyewaongoza watu wangu kupitia nyikani, Yule pale," na kuliita Jina Lake "Yesu."

206 Kutoka kwa "MIMI NIKO," Yeye alikuwa ndiye MIMI NIKO. Na "MIMI NIKO" ni asiye na mwisho, ni wa Milele. Si "Nilikuwa, nitakuwa." Bali "MIMI NIKO," wakati uliopo, nyakati zote, "yeye yule jana, leo, na hata milele."

207 Ndipo Paulo akalia kwa sauti kuu, "Bwana, ninataka kuwekeza. Wataka nifanye nini? Utanifanya nifanye nini, Bwana? Nifanye nini?" Loo, jamani! "Naweza kufanya nini?"

208 Ndipo akaenda huko chini Arabia kwa miaka mitatu na nusu, na kuchukua Maandiko, apate kujua kama Huyo hakuwa Mungu yeye yule. Ndipo akarudi. Na yote ambayo amefundishwa kufanya, ninii yake yote—madhehebu yake yalikuwa yamemwondokea, ninii vyake vyote—vipaji vyake vya elimu yake.

209 Ndipo akasema, katika Wakorintho pale, "Kamwe sikuja kwenu kwa maneno ya kielimu, kwa sababu mngewekea msingi ninii yenu . . . nyinyi—mngewekea msingi mawazo yenu juu yangu, ya kuwa mtu mwenye elimu, mtu mashuhuri. Bali nilikuja kwenu kwa nguvu na madhihirisho, madhihirisho ya Roho Mtakatifu." Kama hilo si jambo lile lile Yesu alilosema katika Marko 16, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili," inamaanisha kudhihirisha Nguvu! Maana, kuhubiriwa tu kwa Neno, pekee, hakutalileta. Inakubidi kulikubali Hilo, kisha Hilo linadhihirisha, "ishara hizi zitafuatana nao," kwa sababu ni Neno. Mnaona?

210 Sasa tunaona ya kwamba Paulo, basi, ilimlipa, na Uzima mkuu wa Milele.

Ni uamuzi wa kipumbavu jinsi gani sasa!

211 Ninafunga, Mungu akinisaidia. Ninyi ni wasikilizaji wazuri sana. Ninajua nimeuchosha uvumilivu we—wenu. Samahani. Lakini ni kujaribu tu, mimi . . .

212 Sistahili kusimama hapa ku—kuzungumzia jambo kama hili. Ni zaidi. Si—siwezi, siwezi kujifikisha mahali hapo, na ni—ninajiweka mwenyewe kuwa mwalimu. Ni—nisingeweza kufanya hivyo, kwa sababu si—si—sina maarifa ya kielimu. Bali ninao ufunuo ambao uko hasa na Neno, nalo Neno linarudi kuishi na kuzaa kile Hilo linachosema litafanya. Mnaona? Mnaona? Wala na wale mitume; ni Paulo tu, naye alisema ilimbidi kusahau yale mambo aliyojua, mnaona, ili kuwekeza.

213 Na labda huenda ikakubidi kusahau hayo, "Mimi ni *fulani-wa-fulani*. Mimi ni mfuasi wa hili. Mama yangu alikuwa mfuasi wake." Huenda ikakubidi kusahau hilo, ikiwa unataka kuwekeza. Kwa hiyo si ingekuwa ni pupa? Usingetaka kufanya kama huyu kijana mfanyabiashara, ni jambo la kijinga jinsi gani jamaa huyo alilofanya alilipouacha uwekezaji kama huo.

214 Hilo, sasa, mimi sikuombi kuwekeza pesa zako. Hiyo ni juu yako, unachofanya na hiyo, kwa shirika fulani la kimishenari, ama chochote kile, kuwatuma wamishenari. Sijui kuhusu hilo. Mungu atashughulikia hilo.

215 Ninazungumza nanyi juu ya hati ya mkataba wa Uzima. "Njoo, unifuate. Chukua msalaba wako. Acha kila mtu akuite kile watakacho; lakini wewe—wewe njoo, unifuate." Sasa yeye hakuwa tayari sana kufanya jambo hili. Alifanya jambo la kipumbavu sana, vile vile tu kama watu wa Wakati wa Laodikia leo, katika hati ya mkataba. Hawako tayari. Hawataki.

216 Hiyo ni kama yule kijana tajiri. Vipi kama ningeweza kumfuata kwa dakika chache tu? Hebu tufanye tu kwa dakika moja, angalieni. Chache, muda kidogo tu baadaye, tunamwona jamaa huyu kijana tajiri. Hebu tuangalie mwisho wake, na kisha tutafunga. Mwangalie. Tunamfuata, na yeye alikuwa mfanyabiashara. Na biashara yake ilinawiri!

217 Kwa hiyo, enyi wafanyabiashara, kumbukeni, ufanisi haumaanishi kila mara kwamba wewe ni Mkristo. Ibilisi . . . Mwajua, Daudi, ninaamini, wakati mmoja alisema, "Niliwaona waovu wakistawi kama mti wa kijanikibichi, lakini Mungu akasema, 'Je! uliwahi kumwangalia mwishowe?'" Hiyo ndiyo tofauti. Angalia kwenye mwisho wa safari.

218 Ern Baxter, mmoja wa wenzangu, mtu mwenye maadili mema sana. Wengi wenu mnamfahamu Ern, mhudumu mzuri sana, mwenye kipaji, wa Kanada. Alikuwa akiniambia hadithi ndogo, siku moja. Akasema, "Ndugu Branham, tunaendesha baiskeli." Kisha kasema, "Nilipokuwa mtoto, tungeweza, ningeenda katikati ya mji, ninunue kifurushi cha vyakula kwa ajili ya mama yangu, na hata nisiguse u—usukani wa baiskeli

yangu. Ndipo kampuni hii ikaja kule, jina lake Schwinn, ilikuwa inaenda kutoa baiskeli kwa mtoto yeyote angeweza kuendesha kwenye ubao wenye upana wa futi moja uliosimama urefu wa futi mbili hewani, kwa yadi thelathini." Kisha akasema, "Kila mmoja wetu alijua ya kwamba tungeweza kufanya hivyo."

219 Tena kasema, "Kulikuwako na mvulana mmoja mdogo dondoadume pale. Hata tusingeweza kushirikiana naye, kwa sababu ha—hakuonekana kama alijua mengi sana," akasema, "kwa hiyo tulifikiria tulikuwa wa tabaka bora kidogo tu kuliko alivyokuwa. Naye alifaulu, ama alitaka ku—kuingia mashindano, pia." Ndipo kasema, "Unajua nini? Kila mmoja wetu alianguka kutoka kwenye ubao huo, isipokuwa yeye." Kisha akasema, "Yeye aliiendesha moja kwa moja hadi mwisho, ndipo akashuka na kuinama, akaichukua baiskeli yake ya Schwinn na akaanza kuendesha akiondoka." Tena kasema, "Sisi wavulana tulikutana naye huko chini pembeni, na tukasema, 'John, tu—tunataka kujua. Ulifanikiwaje?'"

220 Akasema, "Vema, sasa, enyi wavulana, nitawaambieni kilichotendeka." Kasema, "Niliangalia kile nyinyi nyote mlichofanya, nami nikaenda njia nyingine." Kasema, "Mnaona, mlipoipanda nao wakawasukuma, mlikuwa bora zaidi. Nyinyi nyote mu waendeshaji bora kuliko mimi, mnajua hilo," kasema, "kwa sababu siwezi kuendesha bila ya kushikilia usukani."

221 Wala nami siwezi kwenda pasipo kushikilia Msalaba, mnaona. Neno hili halina budi kuwa ndilo Maisha yangu. Hilo ndilo yako yanahitaji. Si—si—siwezi—siwezi kunena bila usukani huu kuongoza, huyu Roho Mtakatifu ambaye hunisogesha na kuniongoza.

222 Alisema, "Siwezi. Mimi—mimi—mimi si mwendeshaji kama mlivyo nyinyi jameni. Lakini," kasema, "ninaona mahali mlipofanyia kosa lenu. Mlikuwa mkiangalia chini namna *hii* na kujaribu kuiweka sawa." Kisha kasema, "Hilo liliwafanya kuwa na wasiwasi na mkaanguka." Akasema, "Nilipopanda pale, nao wakanisukuma, niliendelea tu kuangalia mwisho wa safari na nikashikilia imara."

223 Sasa, enyi wafanyabiashara, msiangalie *hapa*, biashara yenu inaweza kuhisi, kuanguka kesho, huenda ikaanguka siku nyingine, lakini angalieni mwisho wa safari, na huko ndiko hati yenu ya mkataba itakapoleta faida.

224 Jamaa huyu mdogo alipata mali nyingi zaidi, bali tunaona hatimaye siku yake ya malipo iliwadia. Ulafi wake, mali iliongezeka sana mpaka akakuta kwamba ilimbidi kujenga maghala mapya. Loo, biashara yake ilizidi kupanuka! Aliendelea kuwa mfuasi wa kanisa. Unasema, "Ndiyo?" Naam, ndugu, hiyo ni kweli. Aliendelea kuwa mfuasi wa kanisa. Basi usiku mmoja, alikuwa mkubwa sana, hata kulikuwako na mtu aliyekuwa maskini katika roho . . .

225 Mwajua, si lazima tuwe maskini sana katika fedha, itatubidi kuwa maskini katika roho. Yesu alisema, katika Mathayo 5, "Heri walio maskini katika roho, kwa kuwa ni wao," si dhehebu, "Ufalme."

226 Basi maskini wa roho alikaa langoni pake, naye akampa makombo machache. Kwa maneno mengine, walipopita pale, huenda alimpa kitu katika kisanduku cha mchango, ama kitu fulani. Ama huenda alisema, "Unajua, hao ni watu wazuri, sina kitu dhidi yao. Nitaenda kwenye kiamshakinywa chao, mara moja moja." Utatoa makombo machache. Hilo huenda likawa hivyo. "Loo, mke wangu ni mshiriki huko chini. Lakini mimi, mwenyewe, unaona, ni—ninapendezwa na wadhifa wa—wa—wangu pamoja na wafanyabiashara wenzangu, unaona." Naye akafagilia mbali hayo makombo.

227 Naye Lazaro, maskini wa roho, alilala pale bila hata dawa ya kutosha kujishughulikia mwenyewe, nao mbwa wakaramba kidonda chake. Lakini usiku mmoja, yeye, wote wawili wakafa. Na walipokufa, Biblia ilisema kwamba yule maskini wa roho "alibebwa na Malaika wabeba jeneza, wakampeleka kwenye kifua cha Ibrahimu," mmoja alikuwa amewekeza, akamfanya Yeye uwekezaji wake katika Uzima wa Milele. Yeye hakuishia yale aliyokuwa nayo hapa. Kwa ajili ya umaarufu wake, hakuwa nao. Alikuwa ombaomba langoni. Yeye, hakuwa na kitu. Hakuwa na pesa. Hakuwa na chochote. Hakuwa na marafiki. Lakini, hata hivyo, alikuwa mwaminio. Alikuwa amefanya uwekezaji wake. Naye akafa mtaani, huku mbwa wakiramba vidonda vyake. Nayo Biblia ilisema, kwamba, "Malaika walimbeba wakampeleka kwenye kifua cha Ibrahimu."

228 Basi usiku uo huo, yule tajiri, mtawala mzee sasa, alikuwa amekuwa na maisha makuu ya ufanisi, naye akafa. Sasa yeye alilipa katika mgao wa faida, pia. Mhubiri fulani wa kiakili akaja, labda akiwa amepindua ukosi wake, na—na labda amevaa majoho yake yote ya kikuhani, naye akasema . . . Nao wakapandisha bendera nusu mlingoti, na, nayo maua yasingalitoshea kwenye bwalo hili la dansi hapa. Na, loo, walikuwa na sherehe kubwa jinsi gani, na shughuli zote. Labda rais wa shirika la benki, na hao wote, walikuja, nao walikuwa wabeba jeneza wake. Basi labda mhudumu huyo wa kiakili alisimama na kusema, "Ndugu yetu wa thamani, ni mara ngapi ameandika hundi kwa ajili ya wajane, na ni mara ngapi yeye amelipia dhehebu letu kuu na kudhamini mradi wetu!" Na labda wafanyabiashara walisimama na kutoa hotuba. Alipata thawabu yake. Hiyo ni kweli. Uwekezaji wake ulilipa namna hiyo. Lakini, kutoka ulimwenguni, yeye alikuwa ni mtu mashuhuri.

229 Bali kwa sababu kwamba yeye alikataa ule uwekezaji ambao Yesu alimpa, Biblia ilisema, "Kuzimuni yeye aliinua macho yake." Ndipo akamwona mtu yule aliyekuwa amewekeza

vinginevyo, akiwa salama katika kifua cha Ibrahimu, amefarijika, akitembea huko, mzima. Ndipo akalia. Sasa angalieni. Mnasema, hivi yeye alikuwa Mkri-. . .? Naam. "Baba Ibrahimu," Myahudi, kweli, "Nakuomba, mtume Lazaro, maskini wa roho, aliyewekeza. Niliukataa Huo. Lakini mtume Lazaro na maji kidogo tu, miale hii inanitesa."

Akasema, "Mwanangu, ulikuwa na nafasi." Alikuwa nayo.

230 Yesu alimkabidhi. "Uza uliyo nayo, kisha uje, unifuate Mimi. Fanya uwekezaji wako katika—katika Hili. Chukua msalaba wako." Bali ulikuwa ni mkubwa mno.

231 Akasema, "Sasa yeye amefarijiwa, na wewe unateseka. Na kando na haya yote, kuna shimo kubwa lililowekwa kati yako na yeye, ambalo hakuna mtu aliyewahi kuvuka ama atakayepata kuvuka."

232 Hiyo ni kusema, inavunjilia mbali toharani na mafundisho haya yote. Huyo alikuwa ni Yesu Kristo aliyesema hivyo. Usingojee muda mrefu kupita kiasi, ewe bwana. Ndugu yangu wa thamani, uliyepotea, uliyeanguka kutoka kwa Kristo, usingoje muda mrefu kupita kiasi kufanya uwekezaji huu. Huenda alikusudia kufanya hivyo siku moja, bali kama ule msemo wa kale wa Kusini ulivyo, "Kuzimu kwenyewe kumepambwa kwa makusudio mema." Mnaona, makusudio hayafanyi hilo. Soma maagizo yaliyo kwenye chupa, lakini basi kunywa dawa kama unataka matokeo. Fanya uwekezaji wako. Andika jina lako, katika Damu Yake, juu ya moyo wako. Unaona?

233 Tazama, mwangalieni. "Kuzimuni aliyainua macho yake." Alikuwa amelipwa. Halafu basi angalia, yeye alisema, "Basi, Baba Ibrahimu, ikiwa huwezi kufanya hili; usiwaache wenzangu, ambapo urithi wangu wote ulirudi duniani, uwekezaji wangu niliofanya, waambie wasifanye kosa lile lile nililofanya."

234 Je! huenda hiyo ikawa ni wewe, asubuhi ya leo, rafiki yangu wa Kiyahudi ama rafiki Mmataifa? Usiwe na pupa kama jamaa yule alivyokuwa.

235 Akasema, "Mtume huko, na ninaomba wapelekewe ujumbe huu." Loo, alitaka kuwa mhudumu wakati huo. Alitaka kuukubali Huo. Ilikuwa imechelewa kupita kiasi; hawezi kufanya hilo sasa. Wakati wake, yeye alikuwa na nafasi, bali hakuwekeza.

236 Ndipo akasema, "Wanao manabii, wana kile Neno lilichosema, na torati."

237 Akasema, "Naam, lakini kama mtu akifufuka kutoka kwa wafu, na ingeweza kuthibitishwa kwamba alifufuka kutoka kwa wafu, ndipo wataamini."

238 Akasema, "Hawataamini hata mtu akifufuka kutoka kwa wafu."

239 Na miaka elfu mbili imepita tangu tukio hilo. Katika 1963, Mtu yuko miongoni mwetu asubuhi ya leo, akithibitisha kwamba Kristo amefufuka kutoka kwa wafu. Nao Uhai uliokuwa ndani Yake umo ndani ya Kanisa Lake, ukifanya mambo yale yale, kutimiza Neno Lake. Hivi wewe, ndugu yangu, dada, hutafanya uwekezaji huu asubuhi ya leo? Yatoeni maisha yenu kwa Kristo, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa uchaji.

240 Hebu maneno haya yasiwe ni bure, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili." Huna budi. Sasa, sizungumzii kwamba huenda ukapiga makelele, ukapaza sauti, ukanena kwa lugha. Ninamaanisha kuzaliwa mara ya pili, kweli, pamoja na kule kuungama dhambi kwa kilindi. Kwamba hujawahi kuweza, ingawa daima umeshikilia dhehebu lako, ingawa unajua yalikuwa kinyume na Neno, bali hata hivyo kwa ajili ya mawazo ya kibinafsi, na kwa ajili ya kiburi, na kwa ajili ya umaarufu, umebakia katika kanisa hilo kubwa. Hukutaka uhusiano wowote na ile misheni kwenye kona. Unaona, hapo palipo na hazina zako, ndipo ulipo na moyo wako pia.

241 Loo, enyi wafanyabiashara, asubuhi ya leo, ninawatolea, kama wakala wa Yesu Kristo, Uzima wa Milele, hati ya mkataba wa Uzima wa Milele, huyo Kristo Bwana wangu, na Bosi wangu mkubwa, kwa kuwa nimekufa kwa mambo ya ulimwengu, nipate kuishi Kwake pekee. Tukitumia sio mawazo yetu wenyewe, bali kuruhusu tu nia Yake, sisi ni wafungwa, kama Paulo, kama Musa. Haijalishi kile mtu mwingine yeyote anachosema, wewe umefungwa kwa hilo Neno. Roho Mtakatifu huongoza; Yeye hukataza kwenda mahali mahali, Yeye hukataza kuja hapa, Yeye—Yeye hukutuma mahali usingetaka kwenda, na kukukataza mahali ambapo ungeenda. Hivi unataka hati ya mkataba? Unataka kuwekeza?

242 Sasa hakuna mahali hapa kwa ajili ya, kama vile Wamethodisti na karibu Wapentekoste wote wanavyouita, wito wa madhabahuni. Bali hayo ni madhabahu papo hapo unapoketi. Biblia ilisema, "Wote walioamini, walibatizwa." Na kama unataka kufanya maungamo, na unajua kwamba umekuwa makosani, nawe ungetaka kuwa na moja ya hati hizi za mkataba, na ungetaka. Nami ninatumaini huwazii sasa ya kwamba mimi. . .natumai halisikiki la kukufuru ninaposema, "hati za mkataba." Ninatoa tu tamshi hili kulingana na fungu langu. Na wewe ni. . .na—na wewe unataka kuwa na Uzima wa Milele, na unataka kuyawekeza maisha yako katika Yesu Kristo, kama ungetaka sasa, waza kwa nguvu.

243 Sasa, kulingana na sayansi, nguvu za uvutano huishikilia mikono yako chini. Bali kuna uhai fulani ndani yako, unaoweza kuenda kinyume cha nguvu za uvutano, na unaweza kuinua

mkono wako. Na ikiwa uhai huo ndani yako unakwambia, asubuhi ya leo, kwamba kama yule kijana tajiri mtawala, "Ingawa nimekuwa mwanaume mzuri, ama mwanamke, bali si—sina hiyo hati ya mkataba. Ni—nina hakika ya jambo hilo. Nami ni—ninaitaka, hata hivyo." Na kwa Muumba aliyepo, Yule ambaye hunena na anajua moyo, na unajua Yeye angeweza kulitaja jina lako sasa hivi, lakini Yeye anafanya hivyo kwako. "Na basi kwa sababu Wewe unanipa nafasi hii asubuhi ya leo, Bwana, ninakuinulia Wewe mikono yangu. Nirehemu, Bwana. Sitaondoka kwenye bwalo hili la dansi, asubuhi ya leo, Mfarisayo mtupu, mkavu. Ninakubali mpango wako. Ninaukubali Uzima Wako ndani ya wangu. Nitayaacha maisha yangu. Nitafanyika mfungwa kwa Neno Lako."

244 "Niombee, Ndugu Branham. Ninaiinua mikono yangu, kumwonyesha Mungu; si kwako, Ndugu Branham, bali kwa Mungu ambaye yupo. Ninataka uwekezaji huu."

245 Mwaweza kuinua mikono yenu sasa, wakati kila kichwa kimeinamishwa na kila jicho limefumbwa. Mungu awabariki ninyi watu. Haijalishi kama wewe ni . . . Ninawaona wahudumu. Hiyo ni sawa. Iweni wanyofu. Mnaona, wahudumu hawajaachwa. Kusema kweli, hao ndio wachungaji, wanapaswa kuwa ndio wa kutangulia. Vema. Kungekuwako na mwingine kabla sijaomba? Naam, Mungu akubariki. Mungu akubariki, huko juu kwenye roshani. Akubariki. Naam, Yeye anaona mikono yenu, kila mahali. Sasa kwa uaminifu, mnapoiweka mikono yenu chini, mmefanya uamuzi wenu sasa.

246 Sasa ninapoomba na kumwomba Mungu huyu mkuu Yule aliyedhihirishwa katika mwili, na sasa ametolewa tena kwetu, katika umbo la Roho Mtakatifu, naomba Yeye aje moyoni mwako na kulitatua hilo swali milele, na kuandika "amesamehewa" kwenye kitabu cha maisha yako, na kuliandika jina lako katika Kitabu cha Uzima, na kukupa Uzima wa Milele na hakikisho la ufufuo, kwa sababu Kristo atafufuliwa ndani yako. Yule mmekuwa mkimwona akitenda kazi katika mikutano juma hili, akileta na kuthibitisha, akiwafufua wafu, kuwaponya wagonjwa, anazijua siri za moyo, anatabiri kila kitu kikamilifu, ambacho kinatimia, mwaka baada ya mwaka, na hakuna kosa hata moja, Hilo ni Neno. Na ninii . . . Yesu alisema, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu haliwezi kushindwa." Hiyo ndiyo sababu Hilo halishindwi, ni Neno lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huu.

247 Baba wa Mbinguni, wakati wa jioni unaendelea. Tunajua, katika Biblia, kwamba Wewe ulikuwa ule Mti wa Uzima uliotoka kwenye bustani ya Edeni. Nasi tunajua kwamba Maserafi waliuchukua upanga wa Moto, Mwali, wakaulinda huo Mti. Maana, kama mtu angewahi kuugusa Mti huo na kula kutoka Kwake, angeishi milele. Uliulinda Mti huo wakati huo. Bali Moto ule ule, kutoka kwenye ule upanga, Neno la Mungu,

linawaelekeza watu kurudi kwenye Mti huo, huo Mti wa Uzima uliokuja duniani vizuri sana, uliozaliwa katika hori, juu ya zi—zizi ambapo ng’o—ng’ombe na kondoo walikuwa—walikuwa wamelalia na walikuwa wamelala, huku mtoto Yehova akilia, kwa mfano wa Mtoto mchanga. Loo, linapaswa kuwa ndilo jambo ambalo lingeusisimua moyo wa kila mwanamume na mwanamke.

248 Ndipo, basi, Yehova akifa msalabani, akiteseka kwa dhambi za ulimwengu. Haikumbidi kufanya hivyo, bali Yeye alilifanya. Neema Yake ilimshurutisha. Upendo Wake, “Mungu alipenda sana,” na upendo Wake ukamshurutisha, kwa sababu hili lilikuwa—ilibidi jamii hii ya wanadamu kuonyesha sifa Zake za kuwa Mwo—Mwokozi. Ilibidi wapotee. Hakukuwa na kitu kilichopotea; Yeye alifanya vitu kikamilifu. Bali Shetani aliingizwa na kupotosha kile Yeye alichokuwa amekifanya kikamilifu, kwa msingi wa uhuru wa kujichagulia waliokuwa wamewekwa. Halafu basi ilimbidi Yeye kukikomboa, na Yeye akakikomboa.

249 Ee Mungu wa Milele, njoo katika rehema na unenee kila moyo hapa. Pia jalia, leo hii, wakati mikono hii ilipoinuliwa, na labda wengine ambao kwenye wakati huo nilipouliza, hawakuwa na hi—hisi halisi, bali sasa wanayo. Jalia watie sahihi kwa damu ya maisha yao wenyewe, Mungu, ili kuanzia leo na kuendelea, kwamba wanafanya uwekezaji wao wa maisha yao yote, kwa Yesu Kristo na kwa Neno Lake.

250 Na ule Mti mkuu, ule Mti mkuu wa Uzima, wakati Yeye alipokuja duniani, waliukatilia mbali na mkuki wa Kirumi, na kuutundika kwenye mti wa Kirumi, mti katili, uliolaaniwa, bali mle ndani Yeye aliukomboa Mti wa Bibi-arusi, Mti wa Bibi-arusi, mmoja kama Yeye kabisa. Huo Mti wa Hawa kutoka katika bustani ya Edeni, mti uliokuwa umeanguka, Hawa, hapo mwanzo, naye Adamu akatoka akaandamana naye; sasa Adamu anarudi pamoja, Adamu wa pili, akijua kwamba Yeye alikuwa ameyafumbua macho yake, apate kuja kumpokea Hawa Wake.

251 Na sasa kama vile nabii alivyosema, nabii Daudi, alisema atakuwa “kama mti uliopandwa kando ya mito ya maji.” Tujalie, Bwana, kwamba maji ya Uzima yatautia maji Mti huu wa Bibi-arusi katika siku za mwisho, ambapo matawi yote ya kimadhehebu yamepogolewa na mkulima. Na sasa Roho wa Mungu anaishi upya juu ya mti, ambao unatoka kwenye kiini cha huo mti, Neno. Tujalie, Bwana, na jalia wazae matunda mengi. Na jalia hali yao iwe, kama itakuwa kama Lazaro, kama itawabidi kulichukua namna hiyo duniani, tukijua ya kwamba hazina zetu ziko Mbinguni, si za duniani.

252 Wabariki hawa wafanyabiashara, Bwana, hawa wanawake wafanyabiashara, na wote wanaohusika. Nasi tunawakabidhi Kwako sasa, kwa ajili ya kuuendeleza Ujumbe huu. Na

Wewe umeahidi, Bwana, ya kwamba Wewe—ya kwamba Wewe ungetujalia hilo. Na mimi, kama mtumishi Wako, ninawakabidhi Kwako. Pia Wewe ulisema, "Hakuna mtu awezaye kuja wasipovutwa na Baba Yangu." Nao waliinua mikono yao, Bwana. Sasa ninawakabidhi Kwako, kama tunu kutokana na Ujumbe asubuhi hii, wa Neno Lako. Wahifadhi, Bwana, mpaka siku ile. Wewe ulisema, "Hakuna mtu anayeweza kuwatoa mkononi Mwangu. Nami nitamfufua katika siku ya mwisho."

253 Jalia waipokee ile chembechembe ya Uzima, kwamba mbegu iliyorutubishwa ndiyo tu inayoweza kuchipuka, na Maneno ya pekee. Neno la kila mwanadamu limeshindwa, linakufa, halijarutubishwa. Bali Wewe ulisema, "Neno Langu," ambalo ni Biblia, "halitashindwa kamwe." Ni Uzima. Jalia kwamba Uzima uliokuwa ndani ya Kristo utakua kwa Neno, asubuhi ya leo, ambalo wamelipokea. Mimi, kama mtumishi Wako, ninayakabidhi maombi yangu Kwako, kujibiwa katika hili, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

254 Bwana Yesu Kristo awabariki. Ninasikitika sana kuwaweka hapa kwenye saa hii iliyochelewa. Samahani. Lakini kwa kila mmoja mlioinua mikono yenu, hivi mtaniahidi ya kwamba mtaenda kwenye kanisa fulani zuri la Kikristo lililojazwa na Roho wa Mungu? Na kubatizwa katika ubatizo wa Kikristo, ikiwa hujawahi kubatizwa. Chukua mahali pako, ndugu yangu, kwa ajili ya Yesu Kristo.

255 Hata tutakapokutana usiku wa leo, Mungu awabariki. Nayo ibada basi inarudishwa kwa Ndugu Carlson.

63-0803B Uwekezaji
Edgewater Beach Hotel
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org